BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANIWA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2015

## 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2015

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni)**

Kimechapishwa na
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016**

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO


YALIYOMO ........................................................................................ iii
DIBAJI ........................................................................................ iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA KILA MADA ........................................ 2
2.1 KARATASI YA KWANZA ........................................................................ 2
2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi ........................................................ 2
2.1.2 Swali la 2: Qur’an ........................................................................ 3
2.1.3 Swali la 3: Tawhiid ........................................................................ 5
2.1.4 Swali la 4: Fiqh ........................................................................ 6
2.1.5 Swali la 5: Tarekh ........................................................................ 8
2.2 KARATASI YA PILI ........................................................................ 9
2.2.1 Swali la 1: Hoja za Makafiri dhidi ya Qur’an ........................................ 9
2.2.2 Swali la 2: Sura Zilizoteuliwa. ........................................................ 15
2.2.3 Swali la 3: Qur’an Kitabu cha Allah (s.w.) ........................................ 20
2.2.4 Swali la 4: Kuamini Malaika wa Allah (s.w.) ........................................ 24
2.2.5 Swali la 5: Mwisho wa Utume. ........................................................ 30
2.2.6 Swali la 6: Shirk na Madhara yake. ................................................ 34
2.2.7 Swali la 7: Kusimamisha Swala. ........................................................ 40
2.2.8 Swali la 8: Familia ya Kiislamu. ........................................................ 44
2.2.9 Swali la 9: Ndoa na Talaka ........................................................ 49
2.2.10 Swali la 10: Vita vya Uhud ........................................................ 53
2.2.11 Swali la 11: Dola ya Kiislamu baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w.). ... 61
2.2.12 Swali la 12: Maadui wa Dola ya Kiislamu Madina ................................ 66
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA ........................................ 72
4.0 HITIMISHO ........................................................................................ 72
5.0 MAPENDEKEZO ........................................................................................ 73
*Kiambatisho A* ........................................................................................ 74
*Kiambatisho B* ........................................................................................ 75

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya mtihani wa Kidato cha Nne 2015 kwa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, watunga sera, wadhibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi chote cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali zimeainishwa kwa kuonesha watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi. Uchambuzi huu umeonesha jinsi watahiniwa walivyopata alama za juu, kati na chini kwa kila swali na sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri au vibaya zimeoneshwa.

Taarifa hii inaonesha sababu mbalimbali ambazo zilichangia watahiniwa kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi. Sababu zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kuweza kujibu maswali kwa usahihi ni uelewa wa matakwa ya maswali na mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi uliofanyika unaonesha baadhi ya watahiniwa walishindwa kujibu maswali kwa usahihi kutokana na kutotambua matakwa ya maswali na kuwa na maarifa finyu katika mada mbalimbali za somo hili. Aidha, uchambuzi unaonesha kwamba kuna udhaifu mkubwa katika kujibu maswali ya kujieleza, kuhifadhi na kutafsiri Qur'an na Hadithi za Mtume (s.a.w).

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupata ufumbuzi wa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata watahiniwa wa Kidato cha Nne katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika somo hili kitaongezeka.

Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, watahiniwa na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika

kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya mtihani wa Kidato cha Nne hasa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Watahini, Makatibu Muhtasi na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) wa mwaka 2015 kwa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu uliofanyika Novemba 2015 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo hili kwa Kidato cha I – IV. Mtihani huu ulikuwa na karatasi mbili; karatasi ya kwanza ilikuwa na sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali matano ya majibu mafupi (Objective Questions) ambapo watahiniwa walitakiwa kuyajibu maswali yote kwenye karatasi hii. Maswali haya yalikuwa na jumla ya alama 100. Karatasi ya pili iligawanyika katika sehemu A, B, C na D. Kila sehemu ilikuwa na maswali matatu ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu kwa kuandika insha moja kutoka kila sehemu. Kila swali lilikuwa na alama 25 ambapo jumla ya alama ilikuwa 100.

Jumla ya watahiniwa 44,349 waliandikishwa kufanya mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2015. Kati ya hao, watahiniwa 41,200 walifanya Mtihani huu. Idadi hii inaonesha ongezeko la watahiniwa 12,248 ukilinganisha na watahiniwa 28,952 waliofanya mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mwaka 2014. Watahiniwa 21,103 sawa na asilimia 51.2 ya watahiniwa waliofanya Mtihani walifaulu ambapo 19 (0.1%) walipata A, 497 (2.3%) walipata B, 7,104 (33.7 %) walipata C, na 13,483 (63.9%) walipata D. Watahiniwa 20,097 sawa na asilimia 48.8 walifeli kwa kupata F. Kwa ujumla ufaulu wa mwaka 2015 umepanda kwa asilimia 24.67 ukilinganisha na ufaulu wa asilimia 26.55 wa mwaka 2014.

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa maswali ya mtihani na majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Sampuli za majibu ya watahiniwa waliojibu maswali vizuri na ile ya watahiniwa waliojibu vibaya kwa kila swali zimewekwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanyika na kile kilichofanywa na watahiniwa. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ya vizuri, wastani na dhaifu kutegemea na wastani wa asilimia ya watahiniwa waliopata asilimia 30 au zaidi ya alama zilizopangwa kwa swali husika. Mada ilikuwa na ufaulu hafifu kama asilimia ya watahiniwa waliopata wastani wa asilimia 30 au zaidi walikuwa na alama 0 hadi 29, alama 30 hadi 44 ufaulu ulikuwa ni wa wastani na alama 45 hadi 100 ufaulu ulikuwa mzuri.

Mwishoni mwa taarifa hii kumetolewa hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa maswali yote ulivyofanyika. Uchambuzi huu unatarajia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili la Elimu ya Dini ya Kiislamu kwa watahiniwa na hatimaye kuwa na ufaulu mzuri kwa mitihani ijayo ya taifa.

# 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI KWA KILA MADA

## 2.1 KARATASI YA KWANZA

### 2.1.1 Swali la 1: Sunnah na Hadithi

Swali lilikuwa na vipengele kumi (i-x) na lilitahini mada za Sunnah na Hadithi ambazo zilijumuisha: Vitabu vya Hadithi, Mafunzo ya Hadithi Zilizoteuliwa, Historia ya Uandishi wa Hadithi, Uchambuzi wa Hadithi na Umuhimu wa Hadithi na Sunnah. Katika kila kipengele, mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi katika majibu matano (A - E) aliyopewa. Kila kipengele kilikuwa na uzito wa alama 1, hivyo swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 99.7 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu walijibu swali hili. Asilimia 10.6 walipata alama 5 hadi 10, asilimia 39.1 walipata alama 3 hadi 4 na asilimia 50.3 walipata alama 0 hadi 2 miongoni mwao asilimia 3.9 walipata alama 0. Chati Namba 1 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 1: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri. Watahiniwa waliopata alama za juu (10.6%) walionesha kuwa na maarifa katika mada za Sunnah na Hadithi, hivyo kuweza kuchagua majibu sahihi kwa vipengele zaidi ya vitano kati ya kumi vilivyopo kwenye swali. Watahiniwa waliopata alama za wastani (39.1%) waliweza kujibu kwa usahihi vipengele chini ya vitano vya swali. Vipengele ambavyo watahiniwa hao walichagua majibu sahihi ni (i), na (vii) vilivyohusu vitabu vya Hadithi (ii) na (iii) vilivyohusu Hadithi zilizoteuliwa. Ufaulu huo unaonesha kuwa mada zilizotahiniwa katika vipengele hivi zilieleweka vema kwa watahiniwa. Katika kipengele cha (iv) kilichohusu wasimulizi wa Hadithi na cha (x) kilichohusu umuhimu wa Sunnah na Hadithi, watahiniwa walio wengi hawakufanya vizuri kwa sababu katika kipengele cha (iv) walichagua zaidi jibu E badala ya A kwa kuwa walivutwa na umaarufu wa jina la Imamu Bukhari hivyo wakashindwa kukumbuka kuwa Imam Bukhari si Swahaba wa Mtume. Katika kipengele (x) walichagua zaidi majibu A na D badala ya B. Katika majibu hayo kuna neno "mwenendo" lililohusishwa moja kwa moja na tafsiri ya kilugha ya neno Sunnah. Kwa kuliona neno hili watahiniwa wengi walisahau matakwa ya swali ambayo yalihusu kazi kuu ya Sunnah. Watahiniwa wachache (3.9%) hawakuwa na uelewa wa mada zilizotahiniwa kwenye swali hili, hivyo kupata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kuchagua majibu sahihi kwa vipengele vyote 10.

### 2.1.2 Swali la 2: Qur'an

Swali lilihusu mada za Qur'an na lilikuwa na vipengele 15 (i-xv) vilivyobeba uzito wa alama 1 kwa kila kipengele. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuoanisha aya za Qur'an zilizokuwa katika Orodha A na majibu yake katika Orodha B.

Asilimia 99.3 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Asilimia 43.2 walipata alama 7 hadi 15, miongoni mwao

asilimia 0.5 tu ndio waliopata alama zote 15 za swali, asilimia 16.7 walipata alama 4.5 hadi 6.5, na asilimia 40.1 walipata alama 0 hadi 4 miongoni mwao asilimia 5.8 walipata alama 0. Chati Namba 2 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 2: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni mzuri kwa kuwa asilimia 59.9 ya watahiniwa walipata alama 4.5 ambazo zilikuwa ni ufaulu wa wastani kwa swali hili. Ufaulu huo ulitokana na uelewa wa mada za Qur'an hivyo kuwa na maarifa ya kutosha katika Sura zilizoteuliwa na mafunzo yatokanayo na aya mbalimbali za Qur'an. Vipengele vilivyojibiwa vizuri ni:kipengele cha (i) kilichohusu ria katika mali za waislamu, kipengele cha (ii) kilichohusu Mtume kuwa kigezo cha waislamu, kipengele cha (vi) kinachozungumzia ujumbe wa waislamu kuwahusu watu wote, na kipengele cha (xv) kinachusu pango la Hiraa, sehemu ambayo ujumbe wa mwanzo ulimfikia Mtume.

Hata hivyo, wapo watahiniwa (34.3%) waliofanya vibaya katika vipengele (iii), (iv), (v), (xii) na (xiii) na hivyo kupata alama za chini. Kwa kuwa aya kwa vipengele vyote zilitoka katika Sura tofauti tofauti za Qur'an, mtahiniwa alipaswa kuwa na ujuzi wa

Qur’an ili aweze kujibu kwa usahihi. Hii inaashiria kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa kidogo kuhusu sababu za kushushwa aya mbalimbali za Qur’an.

### 2.1.3 Swali la 3: Tawhiid

Swali lilihusu mada za Tawhiid na mtahiniwa alitakiwa kuzipanga sentensi katika mtiririko wenye kuleta mantiki katika vipengele (a), (b), na (c) ambapo kila kipengele kilikuwa na sentensi tano (i - v). Kipengele (a) kilijumuisha sentensi tano tofauti zinazoeleza maana ya dini kwa mtazamo wa kiislamu. Kipengele (b) kilihusu tafsiri ya Suratil-kafiruun inayothibitisha kuwepo kwa dini nyingi duniani na kipengele (c) kilihusu aya za Qur’an zinazoeleza kisa cha Nabii Adamu (a.s) kuhadaiwa na Iblis peponi. Kila kipengele kilikuwa na alama 5 na jumla ya alama zote za swali zilikuwa 15.

Asilimia 98.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Asilimia 29.9 walipata alama 7 hadi 15, miongoni mwao asilimia 0.7 tu ndio waliopata alama zote 15, asilimia 15.4 walipata alama 4.5 hadi 6.5 na asilimia 54.7 walipata alama 0 hadi 4 na miongoni mwao asilimia 33.8 walipata alama 0. Chati Namba 3 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.



Chati Namba 3: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni mzuri ambapo watahiniwa wengi walijibu vipengele vya (a), (b) na (c) kwa kufuata matakwa ya swali. Katika kipengele (b) watahiniwa hao waliweza kupanga kwa usahihi kwa kuwa waliulizwa Sura ya Qur'an inayohusu Tawhiid ambayo husomwa sana katika mada ya Sura zilizoteuliwa. Hii inaonesha kuwa watahiniwa wameihifadhi vizuri Suratil Kaafiruun hivyo waliweza kupanga aya zake kwa usahihi. Hali kadhalika ufaulu wa watahiniwa ni mzuri katika kipengele (c) kwa kuwa kisa cha Nabii Adam (as) ni maarufu. Watahiniwa wengi walishindwa kupanga kipengele (a) kwa sababu kipengele hiki kilihitaji maarifa ya mada ya Tawhiid hasa sehemu ya Maana ya dini kwa mtazamo wa kiislamu, maarifa ambayo watahiniwa hao hawakuwa nayo.

Wapo baadhi ya watahiniwa (33.8%) waliokosa alama katika swali hili kwa kushindwa kufuata maelekezo ya swali. Watahiniwa hao hawakuandika majibu kwa namna ambayo walielekezwa katika swali na waliandika majibu yao kwa mtindo wa namba za kawaida (kiarabu) badala ya Namba za kirumi. Watahiniwa hao walipata alama 0 katika swali hili.

### 2.1.4 Swali la 4: Fiqh

Swali hili lilikuwa na vipengele 15 (a) - (o). Kila kipengele kilibeba uzito wa alama 2, hivyo swali zima lilikuwa na jumla ya alama 30. Mtahiniwa alitakiwa kujibu kwa kifupi maswali yaliyomo katika vipengele hivi. Mada za Fiqh zilizotahiniwa katika swali hili ni pamoja na mambo yanayomuhusu maiti, twahara, maisha ya mwanadamu, Zakat, Swaumu, Swala, Hija, Ndoa na Talaka.

Swali lilijibiwa na Asilimia 99.8 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 21 walipata alama 13.5 hadi 29, asilimia 28.6 walipata alama 9 hadi 13 na asilimia 50.4 walipata alama 0 hadi 8.5 miongoni mwao asilimia 0.1 ya watahiniwa waliofanya

swali hili walipata alama 0. Chati Namba 4 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 4: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri kwa vile wengi (49.6%) wameweza kujibu kwa usahihi vipengele vingi vya swali na kupata alama 9 na zaidi ambazo zilikuwa ni wastani wa ufaulu kwa swali hili. Pamoja na kuwa mada nyingi za swali hili zimegusa maisha ya kila siku ya kiutendaji ya muislamu, yaonesha hata darasani mada hizi zimefundishwa na kueleweka vizuri kwa watahiniwa hao. Vipengele vilivyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi ni (a), (b), (f), (h), (l), na (o). Katika vipengele hivi mada za muhtasari zilizotahiniwa ni Nguzo za Uislamu na Ndoa na Talaka. Watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada hizi.

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (50.4%) walishindwa kujibu vipengele vinavyowataka kutofautisha maneno mawili ambayo yanakaribia kufanana kimatamshi lakini yana maana tofauti (vipengele k na o). Vipengele vingine ambavyo havikufanywa vizuri na watahiniwa hao ni (d), (e), (g), (i) na (n). Kwa mfano; katika kipengele (d) badala ya kutaja masharti ya kutayammamu watahiniwa wametaja hali zinazomfanya mtu aruhusiwe kutayammamu kama vile kuwa

safarini, kuwa mgonjwa na kukosa maji. Kwenye kipengele (e) watahiniwa walipaswa kujua hesabu za sehemu na za asilimia ili waweze kupata mgawanyo wa Zakat ya mazao yaliyolimwa kwa kumwagilia maji na yale yanyeshewayo mvua, ujuzi ambao watahiniwa wengi hawakuwa nao. Pia katika kipengele (g) watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya najisi kubwa na hadathi kubwa na hivyo kuziweka katika daraja moja.

### 2.1.5 Swali la 5: Tarekh

Swali hili lilihusu mada za Tarekh. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua neno au kifungu cha maneno (i) - (xxx) ili kukamilisha sentensi (a) - (o) kwa usahihi. Mada za Tarekh zilizotahiniwa ni Historia ya Mitume Walioteuliwa, Kulingania Uislamu Makka, Upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu, Ushindi wa Waislamu, Kulingania Uislamu Makka na Uanzishaji wa Dola ya Kiislamu Madina. Swali lilikuwa na vipengele 15 na kila kimoja kilikuwa na alama 2 ambapo jumla ya alama zote za swali hili ni 30.

Swali lilijibiwa na Asilimia 99.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 63.5 walipata alama 13.5 hadi 30, asilimia 22.8 walipata alama 9 hadi 13 na asilimia 13.7 walipata alama 0 hadi 8, miongoni mwao asilimia 0.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama 0. Chati Namba 5 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 5: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Ufaulu wa watahiniwa wengi ni mzuri ambapo asilimia 86.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata kuanzia alama 9 ambazo zilikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Wengi wameweza kuchagua majibu sahihi katika kujaza nafasi za vipengele vingi vya swali hili. Hii inaashiria kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali za Tarekh. Vipengele ambavyo watahiniwa wengi wamekosa ni (a), (f), (j), (m) na (o). Katika vipengele ambavyo watahiniwa walikosa, walijibu kwa kuandika majibu ya kubuni ambayo hayakuwemo katika orodha ya maneno waliyopewa.

## 2.2 KARATASI YA PILI

### 2.2.1 Swali la 1: Hoja za Makafiri dhidi ya Qur'an

Swali lilihusu mada ya Ithibati ya Qur'an kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu na liliwataka watahiniwa kujadili hoja zitolewazo na makafiri wakimsingizia Mtume Muhammad (s.a.w) kuitunga Qur'an kwa manufaa yake binafsi na kabila lake.

Swali lilijibiwa na asilimia 60.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu ambapo asilimia 94.6 walipata alama 0 hadi 7, miongoni mwao asilimia 27.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 4.1 walipata alama 7.5 hadi alama 11 na asilimia 1.3 ya watahiniwa walipata alama 11.5 hadi 24 kati ya alama 25 za swali hili. Chati Namba 6 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.



Chati Namba 6: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu. Watahiniwa wengi (94.6%) walishindwa kufikia alama 7.5 ambazo zilikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Baadhi ya watahiniwa hao walielewa kuwa wanatakiwa kuthibitisha kuwa Qur'an ni kitabu cha Allah (s.w.). Hivyo, watahiniwa walijadili hoja zinazopatikana ndani na nje ya Qur'an kama vile Mtume kurekebishwa utendaji wake katika baadhi ya mambo ndani ya Qur'an, Qur'an kujieleza kuwa ni kitabu cha Allah (s.w.) na kutojua kusoma na kuandika kwa Mtume (s.a.w.). Watahiniwa wengine wamejadili hoja za makafiri juu ya namna Mtume alivyoiandika Qur'an na hivyo wakaleta dondoo kama vile: Qur'an ni zao la mwenye kifafa, Mtume aliiandika Qur'an kwa msaada wa mtu aliyejua historia za mitume wa kale, Mtume kunakili vitabu vilivyoitangulia Qur'an na kwamba Mtume alikuwa mtunga mashairi. Hoja zote hizi sio majibu sahihi na hivyo kusababisha watahiniwa hao kupata alama hafifu. Kielelezo 1.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.1**

01. Qur'an ni maneno ya Mwenyezimungu-
(S.w) ambayo aliteremshiwa Mtume wetu -
Muhammad (S.a.w), Kupitia Kwa Jibri (a.s).
Zifuatazo ni hoja ambazo zilitolewa na-
makafiri wakimsingizia Mtume Muhamm-
ad (S.a.w) Kutunga Qur'an Kwa ~~mafu~~ manufaa
yake binafsi na Kabila lake. ambayo ni

Kutojua Kusoma na Kuandika; Mtume
Muhammad (S.a.w) alikuwa haweri Kusoma
wa Kuandisha Kutokana na sababu hiyo
makafiri walikuwa Kumsingizia Mtume, -
Muhammad (S.a.w) Kuitunga Qur'an Kwa
mafaa yake binafsi na Kabila lake

Kutofahamu Kuongea Kabila lingine
zaidi ya Kiarabu; Mtume Muhammad-
(S.a.w) ~~hakiwez~~ hakuweza Kuongea Kabila
lingine zaidi ya Kiarabu kwa sababu ya
Kukua na Kuishi Uarabuni, hivyo Maka
firi walikuwa kumuamini na Kumsingi-
zia Mtume Muhammad (S.a.w) Kuitunga
Qur'an Kwa manufaa yake binafsi na-
Kabila lake.

Kuhifadhi Qur'an Kichwani; Mtume
Muhammad (S.a.w) aliweza Kuitunga -
Qur-ani Kichwani Kwa wepesi na haraka
ambayo ilipelekea makafiri Kuweza -
Kumsingizia Mtume Muhammad (S.a.w)
Kuwa ametunga Qur'an Kwa manufaa
yake binafsi na kabila lake.

Kuitangaza dini ya Kiislamu Kwa


Kutumia Qur'an; Makafiri waliweza kum-
singizia Mtume Muhammad (s.a.w) kuitung
a Qur'an kwa manufaa yake binafsi na
kabila lake, kwa sababu Mtume aliweza-
kuitangaza dini ya Kiislamu kwa kutumia
Qur-an tukufu ya Mwenyezimungu (s.w)
Kutoka na hoja hio Makafiri wali-
weza kudai kuwa Qur'an ni maneno
ambayo aliyatunga Muhammad (s.a.w)
kwa manufaa yake na kabila lake. lakini
si hivyo bali tujuwe kuwa Qur'an ni
maneno ya Allah (s.w).

Kielelezo 1.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeeleza uthibitisho wa Qur'an kuwa ni kitabu cha Allah (s.w) badala ya kujadili hoja zitolewazo na makafiri wakimsingizia Mtume Muhammad (s.a.w) kuitunga Qur'an kwa manufaa yake binafsi na kabila lake.

Uchambuzi zaidi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wachache (1.3%) waliweza kujibu na kupata alama nzuri. Watahiniwa hao walionekana kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya ithibati ya Qur'an kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu kwani waliweza kujadili kwa usahihi hoja zitolewazo na makafiri wakimsingizia Mtume Muhammad (s.a.w) kuitunga Qur'an kwa manufaa yake binafsi na kabila lake. Hoja zilizotolewa na watahiniwa ni pamoja na Mtume (s.a.w) kutunga Qur'an: ili kuleta umoja na ukombozi wa Waarabu, kwa ajili ya kurekebisha tabia ya Waarabu, ili ajinufaishe kiuchumi na ili kuwania madaraka na ukubwa. Kielelezo 1.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 1.2**

1' Qur-an ni kitabu cha mwongozo kilichoshuushwa kwa mtume (s.a.w) kupitia malaika Jibril ili kuwa mwongozo kwa wale wamchao mwenyezi-mungu. Qur-an ina kila nyanja ya maisha na kila mfumo wa maisha unapatikana katika Qur-an. Na yule anayeongozwa na Qur-an amefaulu maisha ya duniani na akhera. Makafiri walimsingizia Mtume Muhammad (s.a.w) kaitunga Qur-an kwa manufaa yake binafsi na kabila lake, zifuatazo ni hoja zinazoonyesha hayo.

Kujinufaisha uchumi: Makafiri wanadai kuwa mtume (s.a.w) alichukulia Qur-an ni kitabu kama vitabu vyengine vinavyoletea watu faida hivyo wananufaika kiuchumi na kuwa na manufaa wao kama wao na ndiyo maana mtume (s.a.w) aliitunga Qur-an ili aweze kunufaika kiuchumi. Lakini hoja hii si sahihi kwani mtume (s.a.w) alikuwa masikini zaidi alipopata utume, pia wakeze walilalamika juu ya ugumu wa maisha, pia mtume (s.a.w) alipotaka kuhongwa ili aache kutangaza uislamu alikataa, si hivyo tu bali mtume (s.a.w) alipokufa zilikutwa dinari saba tu nyumbani kwake, pia alipopewa zawadi alizigawa angekuwa anataka kujinufaisha kiuchumi angezitumia pia zaka na sadaqa alizigawa badala ya kuzirundika.

Kuleta umoja wa waarabu: Hoja hii inahusu juu ya manufaa ya kabila la mtume (s.a.w). Makafiri walisingizia kuwa waarabu hawakuwa pamoja kwani walikuwa wakiishi kwa kujitenga kutokana na kutukuza koo zao hivyo kwa kuwa mtume (s.a.w)

ni mwarabu asingependa yeye kama yeye ni mtume alafu kabila lake halina umoja ndipo alipoitunga Qur-an ili waweze kurekebisha tofauti zao na wawe pamoja lakini hoja hii ni dhaifu kwani katika Qur-an hakuna ushahidi wa aya au sura iliyoshushwa ili iwe ni chanzo cha kuleta umoja wa waarabu, pia mtume (s.a.w) aliletwa kwa ajili ya walimwengu wote itakuwaje alete umoja wa waarabu peke yao, pia mtume (s.a.w) ni swadiqul- Aamin asingeweza kudanganya kwa hilo jambo jema.

Kuwania cheo au madaraka: Hoja hii inaelezea kuhusu manufaa yake mtume (s.a.w) ambapo makafiri walimsingizia kuwa anataka kupata cheo au madaraka kupitia hiyo Qur-an yake aliyoitunga na kwamba watu wakimuamini atapata umaarufu utakaomwezesha kupata madaraka, lakini hoja hii ni dhaifu kwani makafiri wenyewe alitaka kumpa madaraka mtume (s.a.w) ili aache kutangaza dini ya Allah (s.w) lakini alikataa hapo inaonekana kuwa hana haja na madaraka, pia mtume (s.a.w) hakupenda kukwezwa wala kusifiwa na aliwakataza maswahaba wasimsifie na kuwaambia kuwa- "angalieni shetani asiwachezee". Hivyo hoja ni dhaifu.

Kurekebisha tabia mbaya za waarabu. Hoja hii inahusu manufaa ya kabila la- mtume (s.a.w) ambapo makafiri walimsingizia kuwa ametunga Qur-an ili aweze kurekebisha- tabia mbaya za waarabu kwani walikuwa na- tabia za kijahiliya kama kuua watoto wa- kike, kujitenga kwa koo zao, kuuana wao kwa

wao pia walikuwa walovi hivyo makafiri waka-
ona kuwa kwa kuwa mtume (s.a.w) ni mwara-
bu asingependa kuona kabila lake lipo hivyo
ndipo alipoamua kuitunga Qur-an ili aweze kure-
kebisha tabia zao mbaya lakini hoja hiyo ni
dhaifu kwani mtume (s.a.w) aliletwa kwa ajili
ya walimwengu wote na sio waarabu pekeyao,
pia kwa kuwa mtume (s.a.w) ni mkweli na mu-
aminifu asingeweza kudanganya, pia kurekebisha
tabia ni jambo jema asingeweza kutumia uongo.
Makafiri wanaipinga Qur-an si
kwa madai hayo tu bali hata kusema Qur-an ni
zao la mtu mwenye kifafa, mtume (s.a.w) alifu-
ndishwa na padri Bahira, mtume (s.a.w) alifun-
dishwa na Jabir na Yasir, mara Qur-an ni aya
za shetani, mara Qur-an ni matokeo ya kunakili
biblia ambapo hoja zote hizo ni dhaifu.

Kielelezo 1.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeweza kujadili hoja zitolewazo na makafiri wakimsingizia Mtume Muhammad (s.a.w) kuitunga Qur'an kwa manufaa yake binafsi na kabila lake.

### 2.2.2 Swali la 2: Sura Zilizoteuliwa

Swali lilihusu mada ya Sura Zilizoteuliwa na lilipima ufahamu wa watahiniwa juu ya tafsiri ya Suratu dh-Dhuha na kisha kueleza mafunzo sita yatokanayo na sura hii.

Swali lilijibiwa na Asilimia 11.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 68.5 walipata alama 11.5 hadi 25, asilimia 10.6 walipata alama 7.5 hadi 11 na asilimia 20.9 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 5.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Chati Namba 7 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 7: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri kwani asilimia 79.1 ya watahiniwa wote walipata kuanzia alama 7.5 ambazo zilikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Watahiniwa wengi (68.5%) waliweza kuandika tafsiri ya aya zote za Suratu dh-Dhuha na kisha kueleza vizuri mafunzo ya Sura hii. Majibu yao yanaonesha walikuwa wamehifadhi vizuri Suratu dh-Dhuha na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mafunzo yatokanayo na Sura hii. Mafunzo manne yaliweza kuelezwa na watahiniwa wengi ambayo ni Allah kuwa na uwezo wa kuapia chochote katika viumbe vyake kwa umuhimu wa ujumbe anaokusudia kuutoa kwa waja wake, Allah (s.w.) yupo pamoja na waumini pale wanapokuwa katika jitihada za kuusimamisha Uislamu, mwanadamu muda wote aangalie alikotoka na awaangalie walio chini yake na umuhimu wa mwanadamu kuzishukuru neema alizojaaliwa na Allah (s.w.). Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 2.1**

2\. Suratu dh-Dhuha, ni sura miongoni mwa sura
zilizoteremshwa katika mji wa Makka. Sura hii ina idadi
ya aya kumi na moja (11). Iliteremshwa kwa lugha
ya kiarabu lakini inatafsiri yake ambayo ni:-
–Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi
wa rehma mwenye kurehemu.
1. Naapa kwa mchana.
2. Na kwa usiku unapoingia (unapotanda).
3. Hakukuacha mola wako na wala hakuku-
kasirikia.
4. Na kwa hakika wakati ujao ni bora ku-
liko wakati uliopita.
5. Na atakupa mola wako mpaka uri-
dhike.
6. Je, hakukukuta ni yatima akakupa
makazi.
7. Na akakukuta hujui kuongoza ajia
akakuongoza.
8. Na akakukuta fakiri akakutajirisha.
9. Basi yatima usiwaonee.
10. Na wala waulizao usiwakaripie.
11. Na neema za mola wako uzitodithie.
Vilevile sura hii ina mafunzo mbalimbali
ambayo yanatusaidia tupate ujuzi wa mambo mbali-
mbali, miongoni mwa mafunzo hayo ni:-
Kwanza, Mwenyezi Mungu ana uwezo
wa kuapia vile alivyoviumba, katika aya ya
kwanza na ya pili tumeona Allah (s.w) anaapia
mchana na usiku. Lakini mwanadamu yeye
ni kuapa kwa jina la Allah (s.w) peke yake
na si vinginevyo, lakini kiapo kiwe katika
sheria maalumu si kuapa hovyohovyo.

2. Pili, binadamu hana budi kuangalia tabaka
aliloko na lililoko chini yake, kwa tunajifunza
kuwa mwenyezi mungu ndiye anayebadilisha hali
ya mtu kutoka eneo moja kwenda jingine, kupi-
tia mwanadamu kutizama hali yake ya nyuma
na waliko chini yake basi ataweza kumwabudu
mwenyezi mungu kwa mazingatio makubwa.
Tatu, Allah (s.w) ndiye huleta mafanikio
na shida, kutokana na sura hii tunapata funzo
kuwa anayekidhiria raha na dhiki ni Allah (s.w)
peke yake. Hivyo kuomba faraja inabidi tumu-
ombe yeye na si mwingine. Hii itasaidia ku-
pata njia bora ya maisha na hatimaye mafanikio.
Nne, tunawajibu wa kushukuru kila neema
ya Allah (s.w), wanadamu wote wanapaswa
warudi chini na kujidhalilisha mbele ya muumba
kwa kushukuru neema mbalimbali alizotuneemesha,
ambapo njia nzuri ya kushukuru ni kuzidi-
sha ibada mbalimbali za faradhi na sunnah.
Tano, mustakbali wa uislamu ni mzuri na
unajengwa kwa wakati uliopo, uislamu kimeenea
unaridhisha ila, ili ukuwe zaidi, juhudi za
sasa na kuendelea ndio zinazofaa zaidi kuliko
kubakia na kuomboleza visa vilivyopita. Katika
hilo waislamu ni kukaza buti kuliendeleza
gurudumu la uislamu.
Sita, tunawajibu wa kuwasaidia na
kuwatunza wasiojiweza wakiwemo mayatima, ka-
tika maisha ya kila siku kwa ambao hawajiwe-
zi, hivyo basi kuwasaidia ni jukumu letu
kwani hayo ndiyo mafundisho ya uislamu.
Mayatima, maskini, mafukara na wakimbizi

2. kama hayo yanahitaji msaada hivyo ushirikiano-
upatikane.
Waislamu wana kila sababu ya kuhakikisha
kuwa uislamu unaimarika kwani Allah (s.w) ndi-
ye anayesaidia nasi tumuombe msamaha na
msaada ili atuwezeshe kwa kila namna kufikia
lengo hilo.

Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyetafsiri Suratu-dh Dhuha na kisha kueleza mafunzo sita yatokanayo na Sura hii.

Watahiniwa wachache (5.2%) walishindwa kubaini matakwa ya swali hivyo kushindwa kujibu kwa usahihi. Watahiniwa hao waliandika tafsiri ya Sura Nashrah badala ya Suratu dh-Dhuha na kutoa mafunzo sahihi ya Suratu dh-Dhuha hivyo kuweza kupata alama za chini. Ukaribu wa Sura hizi mbili katika maudhui umesababisha watahiniwa hao kuchanganya tafsiri ya Suratu Nashrah na kuweza kuandika mafunzo sahihi ya Suratil dh-Dhuha. Vile vile kulikuwa na watahiniwa ambao hawakuihifadhi Tafsiri ya Suratil ya dh-Dhuha hivyo walishindwa kuandika tafsiri na kutoa mafunzo yatokanayo na Suratil dh-Dhuha. Watahiniwa hao walipata alama 0. Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 2.2**


2. Tafsiri ya Suratul -dh- Dhuha na mafunzo sita.
i Naapa kwa dhuha.
2i Na mchana ukatanga
ii Na kwamba mola walee.

mafunzo ya Sura hii
i ~~ku~~ ~~kuwapa~~ Ambayo mola anayoapia kii ti hupwe
jambo ambalo limeshakwa limemleasiniha au kwa kwa
kuna wakati mzuri wa mchana.
ii kuwapa Kheri mtu ambao wanafanya mambo mema
ya kumtukuza yeye.
iii kuwa kwa Sura hii inatupatia mambo mazuri ambayo
aliyo yaridhi yeye alairidhi yeye kupata neema kubwa.
iv Sura hii inatupasia funzo kwa kuwatendea mayatima
mambo mazuri.
v Sura hii inatupasi funzo kwa mtu atakaye fanya
jambo au mambo mema na kupamikiwa.
vi Sura hii inatupatia funzo kwa mtu atakaye fanya
jambo au mambo maovu hatofanikiwa na kutiwa
katika moto.

Kielelezo 2.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutafsiri na kutoa mafunzo sita ya Suratu-dh Dhuha na badala yake alitafsiri na kutoa mafunzo ya Suratu Nashrah.

### 2.2.3 Swali la 3: Qur’an Kitabu cha Allah (s.w.)

Swali hili lilihusu mada ya kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur’an na lilipima uwezo wa mtahiniwa katika kuibua fikra juu ya Qur'an, ambapo lilimtaka mtahiniwa kueleza hekima sita za Qur’an kushushwa kwa lugha ya Kiarabu.

Swali lilijibiwa na Asilimia 22.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 73.5 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 4.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Asilimia 22.4 walipata alama 7.5 hadi 11, asilimia 4.1 walipata alama 11.5 hadi 25. Chati Namba 8 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 8: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu. Hii inatokana na ukweli kuwa watahiniwa wengi (68.6%) waliofanya swali hili hawakuwa na uelewa wa kutosha wa mada ya Kushuka na Kuhifadhiwa kwa Qur’an kwani pamoja na kubaini matakwa ya swali, hawakuweza kueleza hekima sita za Qur’an kushushwa katika lugha ya kiarabu kwa usahihi. Watahiniwa hao walieleza hekima pungufu ya sita au walizitaja tu na kushindwa kutoa

maelezo yenye mantiki yenye kutetea hoja walizozieleza, hivyo kupata alama za chini sana katika swali hili. Pia kulikuwa na watahiniwa wachache (4.9%) waliopata alama 0 kwa sababu hawakuwa na maarifa ya mada ya kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an. Baadhi yao walieleza ushahidi wa kutoka kwenye Qur'an kuonesha kuwa imetoka kwa Allah (s.w) na pia baadhi yao walieleza nguzo sita za imani badala ya hekima sita za Qur'an kushushwa kwa lugha ya Kiarabu. Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.1**

| | |
|---|---|
| 3 | Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'an kwa ki |
| | arabu ili mpate kufahamu (12:2). Mwenyezi mun |
| | gu ametumia lugha ya kiarabu katika kuwasili |
| | sha kitabu chake kwa waja wake. Njia zilizo |
| | tumika kushushwa ~~k~~ Qur'an ni . |
| | - kushushwa kidogo kidogo kwa muda wa |
| | miaka 23 |
| | - kukosolewa kwa mtume ndani ya Qur'an |
| | - kuandikwa katika magome ya miti |
| | - kuandikwa kwenye majiwe |
| | - kutumwa malaika |
| | - ~~kut~~ ~~kwa~~ kutokujua kusoma na kuandika. |
| | kwanza kushushwa kidogo kidogo kwa mu |
| | da wa miaka 23. Mwenyezi mungu ametumia |
| | njia ya kushusha Qur'ani kidogo kidogo kwa |
| | muda wa miaka 23 enzi za mtume (S.a.w). |
| | pili kukosolewa kwa mtume ndani ya |
| | Qur'ani hekima ya kushushwa Qur'ani ni ku |
| | kosolewa kwa mtume ndani ya Qur'ani hii ni |
| | njia ya hekima ya kushushwa kwa Qur'ani |
| | ya mwenyezi mungu kwa lugha ya kiarabu. |
| | Tatu kuandikwa katika magome ya mi |
| | ti, moja ya hekima ya kushushwa kwa ~~karab~~ |

~~lugha ya Kiarabu~~ Qur'ani katika lugha ya
Kiarabu ni kuhifadhiwa katika magome ya miti
wakati wa mtume (S.a.w).
Nne kuandikwa kwenye majiwe maku
bwa, Miongoni mwa hekima ya kushushwa Qur
ani ni kuandikwa kwa majiwe makubwa amba
yo mtume na masahaba wake waliisoma kwa
lugha ya Kiarabu.
Tano, kutumwa malaika. Miongoni mwa
hekima ya Qur'ani ni kutumwa kwa malaika
kuja kumsomesha mtume (S.a.w) Malaika aliye
kuwa akimuhifadhisha mtume ni JIBRIL ndi
ye malaika mkuu na alofanya kazi hiyo.
Sita, kutokujua kusoma na kuandika
kwa mtume Muhammad (S.a.w). Mtume ali
kuwa hajui kusoma wala kuandika ndipo alipo
tumwa malaika aje amsomeshe mtume (S.a.w)
wakati wa utume wake.
Kwa pamoja, tunaona kuwa hekima
zilizotumika kushuka kwa Qur'ani ni kutokujua
kusoma na kuandika kwa mtume, kwa kutumiwa
malaika, kuandikwa kwenye majiwe, kuandikwa
kwenye ~~to~~ magome ya miti na kushushwa kid
ogo kidogo kwa muda wa miaka 23.

Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa ushahidi kwenye Qur'an kuonesha kuwa imetoka kwa Allah (s.w) badala ya hekima sita za Qur'an kushushwa kwa lugha ya Kiarabu.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (4.1%) waliweza kueleza kwa usahihi hekima ya Qur'an kushushwa katika lugha ya Kiarabu na kupata alama nzuri. Watahiniwa hao waliweza kuzitaja hekima hizo ambazo ni pamoja na Kiarabu ni lugha ya Mtume (s.a.w) na wale alioanza kuwafikishia ujumbe, Kiarabu kinazungumzwa katika eneo kubwa kiasi cha kuweza kueleza kwa ufasaha

matukio yote yaliyoenea duniani, hivyo itakuwa ni rahisi kutafsiri katika lugha nyingine bila kupoteza ujumbe, Kiarabu ni mojawapo ya lugha zitumikazo duniani hivyo Allah (s.w) aliitumia lugha hiyo ili kuufikisha ujumbe kwa ulimwengu mzima, Kiarabu ni chombo cha kuwaunganisha Waislamu wote ulimwenguni ili wadumishe udugu wao na umoja wao kama wanavyotakiwa wawe na Allah (s.w) aliye mjuzi wa kila jambo. Aidha, alijua kuwa ukuaji wa teknolojia za mawasiliano, uandishi, usafiri, na maingiliano ya watu vinakuja kwa kutumia lugha ya Kiarabu ili ujumbe ufike kila kona. Kielelezo 3.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo 3.2**

3

Qur-an ni maneno ya Allah (S.W) aliyomteremshia Mtume Muhammad (S.A.W) ili yaje yawe muongozo kwa watu wote na wanyakati zote, hapa duniani. Qur-an imeteremshwa katika usiku wenye cheo katika lugha ya Kiarabu, kama pale aliposema Allah (S.W)

"Hakika sisi tumeiteremsha Qur-an kwa Kiarabu ili mpate kuifahamu"

Hivyo, Qur-an imeshushwa kwa lugha ya Kiarabu kwa sababu zifuatazo:-

Mtume mwenyewe ni muarabu. Muhammad (S.A.W) alizaliwa katika kabila tukufu la Kiarabu ambalo lilikuwa limeshika uongozi wa Alqaaba kutoka kwa nabii Ismail. Kwa kuwa Mtume mwenye ni muarabu basi ni lazima Qur-an ishushwe katika lugha ya Kiarabu ili aweze kuufahamu ujumbe wa Qur-an na kuweza kuwafikishia wafuasi wake.

Watu waliomzunguka ni waarabu. Watu ambao wamemzunguka Mtume (S.A.W) ni waarabu ambao walitakiwa waupate ujumbe wa Qur-an katika lugha ya Kiarabu Kama Qur-an ingeshushwa katika lugha nyengine isiyokuwa Kiarabu basi ingelikuwa vigumu kwa Mtume mwenyewe kuweza kufahamu ujumbe wala wafuasi wake wasingepata ujumbe huo wa Qur-an.

Qur-an inapatikana katika lugha zote ulimwenguni. Takriban lugha zote ulimwenguni, unaweza kupata Qur-an. Kwa hivyo, hakuna udhuru wa kukosa ujumbe wa Qur-an kwa sababu imefasiriwa katika lugha zote mfano Qur-an imetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kupitia Sheikh Abdulla Saleh Farsy.

Kiarabu ndio lugha ya waislamu. Kiarabu ni lugha -

ambayo inawakutanisha waislamu katika schemu tofauti
Kama katika ibada ya swala, lugha inayotumika ni Kiarabu
Hivyo, ni jukumu la muislamu kujua lugha ya Kiarabu ili
Kuweza kupata ujumbe wa Qur-an katika uasili wake

Kutokana na maendeleo ya Sayansi na teknolojia. ~~M/Mun~~
M/Mungu (S.W) alijua kua kutakuja maendeleo ya Sayansi
na teknolojia, hivyo lugha ya Kiarabu haitakuwa tatizo na
Sababu ya kumfanya muislamu akose ujumbe wa -
Qur-an mfano kupitia vyombo vya habari, mashekhe -
tofauti wahatafsiri Qur-an katika lugha tofauti.

Bara Arabu ndio chimbuko la elimu zote duniani. Asili ya
elimu zote duniani ni kutoka Bara Arabu, kwa sababu
Mitume wote walitumwa walikuwa Bara Arabu ingawaje
walikuja kwa watu wote. Hivyo, lugha ya Kiarabu haitakuwa
Changamoto kwa muislamu kiasi cha kukosa ujumbe wa
Qur-an.

Kiujumla, waislamu tunatakiwa kujifunza lugha ya
Kiarabu na kuanzisha masomo mbali mbali yanayohusu Kiarabu
Kuanzia kwa watoto mpaka watu wazima. Hii itasaidia -
watu kuweza kupata ujumbe wa Qur-an katika uasili
wake.

Kielelezo 3.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza hekima sita za Qur'an kushushwa katika lugha ya Kiarabu.

### 2.2.4 Swali la 4: Kuamini Malaika wa Allah (s.w.)

Swali lilihusu mada ya kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu na lilipima ufahamu wa mtahiniwa juu ya imani ya kuwepo malaika wa Allah (s.w.). Mtahiniwa alitakiwa kuzingatia kazi sita zifanywazo na Malaika ili kueleza jinsi imani juu ya kuwepo Malaika wa Allah (s.w.) inavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanaadamu.

Swali lilijibiwa na asilimia 32.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 41.1 walipata alama 11.5 hadi 25, asilimia 22 walipata alama 7.5 hadi 11na asilimia 36.9 walipata alama 0 hadi 7 na miongoni mwao asilimia 4.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Chati Namba 9 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 9: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wao katika swali hili ni mzuri. Watahiniwa (41.1%) waliopata alama nzuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu hivyo kuweza kujibu kwa kueleza kazi mbalimbali za Malaika na jinsi imani juu ya kuwepo Malaika wa Allah (s.w.) inavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanadamu. Watahiniwa hao walitaja kazi zote za Malaika na kisha walieleza uhusiano wa kuamini kuwepo kwao kunavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanadamu. Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 4.1**

4 Malaika ni viumbe wa Allah (sw) wa ambao
hutumikia Allah (sw) bila ya kuchoka. Na malaika
huwa na sifa kama vile hawali na walala
hawanywi bali humtumikia Allah (sw) kama vile
kumuabudu na kufanya kazi walizopewa. Hivyo
kutokana na kazi zao Binaadamu au mwanaada-
mu jinsi ya imani juu ya kuwepo kwao
inavyoathiri maisha ya kila siku.
Ifuatayo ni jinsi imani imani juu ya kuwepo

4 kwa malaika inavyoathiri maisha ya kila
siku ya mwanaadamu.
Kushika funguo za motoni: Kazi hii hufanyw
a na Malaika Maliki (AS) mwanaadamu anapoamini
kuwa kuna Malaika Maliki (AS) ambaye anashika
funguo za motoni basi anaweza kujiepusha na
matendo ambayo utayafanya utaingia katika
moto mfano kuzini, wizi, na pia kufanya
matendo mema mfano kusali, kufunga, kutoa
zaka. Hivyo kutokana na kazi hiyo ya malaika
Maliki mwanaadamu anaweza kuathiri maisha yake
ya kila siku na kuweza kuwa mcha Mungu
Kazi ya kutoa roho viumbe: Kazi hii
hufanywa na Malaika Ziraili (AS) mwanaadamu
imani ijuu ya kuwepo kwake malaika huu inaweza
kuathiri maisha ya kila siku ya mwanaadamu.
Hivyo mwaadamu anapojua kuwa ipo siku atatolewa
wa roho basi atazidisha kufanya amali njema
kama vile kutoa zaka, kufunga, kusali na kuwa
karibu na Allah kwa kumdhukiri ili apate atolewe
roho yake kwa upole. Hivyo huzidisha kuchamungu
Kazi ya kushika funguo za pepo: Kazi
hii hufanywa na Malaika Ridhiwani (AS) Imani
ya kuwepo kwake inaweza kuathiri maisha ya
kila siku ya mwanaadamu kwa kuweza kuwa
mwanaadamu anapojua kuwa ipo siku binaanadam
u watahesabiwa na wengine kupelekwa peponi
na wengine kupelekwa motoni basi atazidisha
kufanya ibada mbali mbali ili aweze kuingia
peponi Mfano kusoma Qur-ani, kufuata yale
yote aliyoyaamrisha Allah (sw) na kuacha yale
aliyoyakataza kama vile zinaa, riba, wizi.

4 Kazi ya kuuliza wanaadamu maswali makaburini: kazi hii hufanywa na Malaika Munkari na Nakiri(AS) imani juu ya kuwepo kwao imeweza kuathiri maisha ya kila mtu ya mwanaadamu. Mfano Mwanaadam atakapojua kuwa ipo siku atakufa na kisha maisha yake yatakuwa ni ya kaburini (Barazakh) na akiwa huko atauliza maswali basi atazidisha kukithirisha ~~m~~ kufanya matendo mema na kuweza kuwa mwanaadamu anamcha mola wake ili apate kuweza kuyajibu maswali kwa uzuri. Huyo mwanaadamu inampeleka kumcha mola wake na kila wakati kuweza kumuabudu.

Kazi ya kuandika amali njema na ovu wanazofanya wanaadamu: kazi hii hufanywa na Malaika Rakib na Atid(AS) imani juu ya kuwepo ~~kuwa~~ kwao inamuathiri mwanaadamu ~~kw~~ kwa kuzidisha kumkumbuka mola wake kwa kumuabudu na kufuata yale aliyoamrisha mfano sala, funga, kutoa zaka na sadaka na kuacha yale aliyoyakataza mfano ulevi, wizi, riba, zinaa. Huyo mwanaadamu anapojua kuwa kuliani na kushotoni kwake yupo Malaika basi atazidi kufanya amali njema ili kitabu chake kiwe kizuri na kuacha kufanya amali ~~mbaya~~ mbaya mfano kusengenya, zinaa ~~n~~ ili kitabu chake kiwe kizuri

Kazi ya kutoa wahyi kwa Mitume: Kazi hii hufanywa na malaika Jibrili (AS). Kazi hii inaweza ya kuamini kuwepo kwa Malaika Jibrili (AS) inaweza kumwezesha ~~k~~ mwaadamu kujua kuwa Allah (SW) humtumia malaika huyu kupeleka wahyi kwa mitume ili Mfano mtume ~~SW~~ (SAW)

| | |
|---|---|
| 4 | alikuwa akipelekewa wahyi na Jibril (AS) hivyo |
| | ~~mwanado~~ mwanaadamu anazidi kupata imani |
| | juu ya kuamini ~~malai~~ Mitume na kuyafuata |
| | na kufuata yale waliwamrisha na kuacha |
| | yale waliyoyakataza. mfano Mtume (SAW) alipewa |
| | kitabu cha Qur'ani ambacho anachushuwa na |
| | Allah (SW) kupitia Malaika Jibril (AS) hivyo mwana |
| | adamu anaweza kuamini Qur'ani. |
| | Hivyo imani juu ya kuwepo Malaika |
| | pamoja na kazi zao imeweza kuathiri maisha |
| | ya kila siku ya ~~mwana~~ mwanaadamu. Hivyo |
| | tunatakiwa tudhidishe kufanya amali njema |
| | ili kesho akhera tupate maisha mazuri pamoja na |
| | hapa duniani |

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza jinsi imani juu ya kuwepo Malaika wa Allah (s.w.) inavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Watahiniwa waliopata alama za chini (32.1%), hawakuwa na uelewa wa mada ya kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu. Watahiniwa hao walishindwa kutoa maelezo sahihi jinsi imani juu ya kuwepo Malaika wa Allah (s.w.) inavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanadamu na hivyo kupata alama za chini. Watahiniwa hao walitoa dondoo pungufu ya sita na pia kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza katika baadhi ya dondoo. Wapo baadhi ya watahiniwa (4.9%) ambao walishindwa kutambua matakwa ya swali kwa kuwa hawakuelewa maana ya neno “inavyoathiri” katika swali hili hivyo kupata alama 0. Watahiniwa hao walitafsiri neno “Inavyoathiri” kwa maana ya madhara. Maelezo ya watahiniwa hao yalimtaka mwanadamu kuchukua tahadhari asije kuathirika na kazi yoyote miongoni mwa kazi za Malaika kinyume na maana halisi ya swali. Kielelezo 4.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa mujibu wa maelekezo ya swali.

**Kielelezo 4.2**

4\. Kupuliza parapanda ni Moja kati ya kazi za Malaika.

Hoja zifuatazo ni juu ya imani juu ya Kuwepo Kwa Malaika inavyoathiri Maisha ya kila Siku ya Mwanadamu.

IMani potofu. Mwanadamu anakuwa na Imani potofu kwa sababu haamini kama Malaika wapo na kama Malaika hao wanaweza Kufanya Kazi hizo walizopewa na Allah Subuhanahu-wataaalah. Yaani Wanaadamu wanakuwa na ile Imani potofu juu ya Kuwepo kwao kwa hao Malaika.

IMani Potofu Kuhusu uwepo wa Malaika hao. Wanaadamu wanakuwa na ile Imani ya Kutokuamini Vitabu vya Mwenyezimungu Pamoja na Uwepo wa Malaika wa Mwenyezimungu Kwa hiyo Wanaadamu tusiwe na imani hiyo potofu Kwani itatupeleka pabaya Siku ya Mwisho. Kwa sababu imani hii potofu ~~imewa~~ imewafanya baadhi ya Wanadamu ambao ni Waislamu Kuritadi katika Uislamu Kutokana na Upotofu wa Imani yao

IMani Potofu Kuhusu Kazi za Malaika. Wanaadamu hawaamini zile kazi zinazofanywa na Malaika hao Kutokana na Imani potofu waliyo nayo. Hiyo itapelekea Wanaadamu Kwenda Mahala pabaya Kabisa Kinyume na taratibu za Kiislamu.

Hivyo ndivyo Wanaadamu walivyoonyesha imani yao potofu Kuhusu uwepo wa Malaika pamoja na Kazi wanazofanya Malaika hao wa Mwenyezimungu. Ewe Mwanadamu Usiwe na Imani potofu Kuhusu Mungu wako pamoja na Malaika wake.

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza imani potofu kuhusu kuwepo kwa malaika badala ya kueleza jinsi imani juu ya kuwepo Malaika wa Allah (s.w.) inavyoathiri maisha ya kila siku ya mwanaadamu.

### 2.2.5 Swali la 5: Mwisho wa Utume

Swali lilihusu mada ya kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu ambapo mtahiniwa alitakiwa kuthibitisha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wa mwisho kwa kutoa hoja tano.

Swali lilijibiwa na Asilimia 35.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 58.8 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 5.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Asilimia 23.8 walipata alama 7.5 hadi 11, asilimia 17.4 walipata alama 11.5 hadi 23.5. Chati Namba 10 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 10: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa kwenye swali hili ulikuwa wa wastani. Watahiniwa wachache (17.4%) walimudu kujibu swali hili vizuri na kupata alama nzuri. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu na pia walielewa matakwa ya swali hivyo kupata ufaulu mzuri. Hoja maarufu zilizobainishwa na watahiniwa hawa ni kukamilika kwa ujumbe wa Uislamu na Mtume Muhammad kutajwa ndani ya Qur'an kuwa ndiye Mtume wa mwisho. Baadhi ya watahiniwa (23.9%) walipata alama za wastani kwa kuwa

walitumia hoja pungufu ya tano kuthibitisha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wa mwisho. Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo 5.1**

5. Mtume ni watu waliotelewa na Allah (Sw) kwa lengo la kutangaza tawhiid. Kwa mujibu wa Qur-an, "Hakuwa Mtume Muhammad (SAW) baba wa yeyote bali alikuwa mtume wa ~~Mwen~~ ~~Mg~~ Mwenyezi Mungu naye ni mtume wa mwisho". Ni kweli ~~A~~ hakuna Mtume baada ya Muhammad (SAW) kutokana na hoja zifuatazo:-

**Mafunzo yake yamekamilika;** Mafunzo yote aliyokuja nayo mtume (SAW) yamekamilika na yanakwenda sambamba na wakati wa sasa. Allah (Sw) anasema katika Kur-ani, "Hakika leo tumekukamilishieni dini yenu". Hii ina maana kwamba mafunzo yote yanayokwenda sambamba na maisha ya mwanaadam yamekamilike na ndio maana hakuna mtume mwengine baada ya Mtume Muhammad (SAW).

**Mtume (SAW) ameletwa kwa umma wote;** Mtume (SAW) amepewa jukumu la kueneza tawhiid kwa watu wote ulimwenguni. Allah (Sw) anasema, "Sema! hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na nimeletwa kwenu nyinyi nyote". Kutokana na hoja hiyo ni wazi kwamba hapana mtume mwengine badala ya Mtume (SAW) kwani yeye ameletwa kwa umma wote.

**Allah (Sw) ameahidi kuyalinda mafundisho yake;** Ahadi ya Allah (Sw) kuhusu kuyalinda mafundisho ya Mtume (SAW) ni pale aliposema, "Hakika sisi ndio

5. tuliyatekeleza mawaidha haya na haki sisi
ndio tutakayoyalinda". Kutokana na hoja
hiyo hapana wala hahitajiki Mtume
mwengine baada ya Mtume Muhammad (SAW)
kwani ahadi za Allah (SW) ni za kweli
Qur-ani yenyewe inathibitisha kuwa
Mtume Muhammad ni mtume wa mwisho
Uthibitisho wa hayo ni pale Allah (SW)
aliposema katika Kur-an tukufu,
"Hakuwa Muhammad baba ~~ya~~ ~~y~~ wa
yeyote bali alikuwa Mtume wa ~~Allah~~
Mwenyezi Mungu naye ni Mtume wa
mwisho". Kutokana na uthibitisho huo
ni wazi kwamba hapana mtume
mwengine baada ya Mtume Muhammad
(SAW).
Mafundisho yake yanatosheleza
mahitaji ya wanaadam; Kikawaida
mwanaadam yeyote huhitaji muongozo
katika maisha yake. Kupitia mafunzo
ya Mtume (SAW) wanaadam wamepata
muongozo wa kuyaendesha maisha
yao ya kila siku. Mfano Mtume (SAW)
ameeleza juu ya ubaya wa shirki
na madhara yake. kupitia Kur-an
"Hakika ya shirki ni dhulma kubwa"
Dhulma hiyo inaweza kuwa ya mtu
binafsi au katika jamii. Kwa hiyo
mafundisho kama hayo yamefanya
kutokuwa na Mtume mwengine baada
ya Mtume Muhammad (SAW) kwani
Mtume (SAW) hasemi kwa matamanio.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa maelezo sahihi kuthibitisha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wa mwisho.

Uchambuzi zaidi uliofanywa kwenye majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi (53.9) waliofanya swali hili hawakuweza kubainisha vizuri hoja zinazothibitisha kuwa Muhammad (s.a.w.) ni mtume wa mwisho na hivyo kupata alama chini ya wastani. Pamoja na kuelewa matakwa ya swali, watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya

kuamini mitume wa Mwenyezi Mungu hivyo kushindwa kujibu swali kwa usahihi. Pia wapo baadhi ya watahiniwa (5.4%) walioeleza nguzo ya kuamini mitume kama ndio hoja ya mwisho wa utume. Watahiniwa hao walipata alama 0 kwa kuwa walieleza sababu za kuwaamini mitume wote wa Allah (s.w) badala ya Hoja za Mtume Muhammad kuwa Mtume wa mwisho. Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa mujibu wa matakwa ya swali.

**Kielelezo 5.2**

5. Hapana mtume baada ya muhamad (s.aw). Hii ili weza kujulikana baadhi ya mitume iliyobakia isingeweza kuitumikia dini vizuri kama aliyotumikia mtume muhamad (s.aw)

Baadhi ya mitume iliyobakia haikuwa waamini ju katika kutoa mafundisho ya dini kwa waislamu. Hii iliweza kusababisha kutokuwepo kwa mitume baada ya mtume muhamad (s.aw) ndiye mjumbe wa mwenyezimungu ambaye alikuwa muaminifu katika Dini yake na kutoa ujumbe kwa Waislamu wote.

Wasingeweza ~~aa~~ kuendeleza dini kama mtume alivyofanya katika kazi yake. Vilevile mitume iliyo bakia haikuweza kusimamia na kuendeleza din kiujumla hii ni kwasababu mtume muhamad (s.aw) ndiye angeweza kusimamia kazi ya Utume wake katika kutoa semina kwa waislam wote na kufanya baadhi ya mitadhara mbalimbali.

Wasingeweza kusimamia ummut Muhamad (s.a.w) kwa kujiepusha na dhambi. Kwani Dhambi zimejaa sana katika dunia na maasi pamoja na maovu yanazidi kuongezeka kila siku mfano Ulevi Uzinzi na Uhuni. Hivi wasingo weza kujiepusha nayo kwa kutoa mafunzo pasipo kutumia Qur-an, Hadithi na Vitabu ambavyo vimeandikwa kwa lugha ya kiarabu na kusolewa tafsrin zake.

Wasingoweza kufikisha ujumbe kama mtume alivyofikisha ujumbe kupitia Qur-an tukufu pamoja na vitabu vilivyoandikwa kwa lugha ya kiarabu. Vilevile mitume iliyobakia haina Uwezo kama mtume muhamad (s.a.w) aliyoweza—


5 kuwa mafundisho ya dini kupitia Qur-an.
Wasingekuwa shupavu kama mtume mu-
hammad (s.a.w) aliyoweza kupambana na kila
matatizo yaliyokuwa yakimtokea. Hii ni kwasaba-
bu mtume alikuwa mjumbe wa mwenyezimungu
na baadhi ya mitume wasingeweza labda kupigana na
vita kama mtume aliyopigania Dini yake na
mpaka sasa dini ipo na watu wanamjua Allah.
(s.w) ndiye mwenyezi mungu aliyeumba kila kitu
Kwahiyo. Hapana mtume baada ya
Muhammad (s.a.w.) Huyu ndiye mtume aliye-
weza kusimamia dini yake kikamilifu pasi
na kuogopa lolote mbele yake.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maelezo sahihi kuthibitisha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wa mwisho. Mtahiniwa alitoa uthibitisho usio sahihi kueleza hakuna Mtume baada ya Muhammad (s.a.w).

### 2.2.6 Swali la 6: Shirk na Madhara yake

Swali lilihusu mada ya Shirk. Mtahiniwa alitakiwa kueleza aina kuu nne za Shirk kisha aoneshe madhara matatu ya Shirk kwa mujibu wa Qur’an.

Swali lilijibiwa na asilimia 30 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 21.6 walipata alama 11.5 hadi 25, asilimia

26 walipata alama 7.5 hadi 11 na asilimia 52.4 walipata alama 0 hadi 7 na miongoni mwao asilimia 5.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Chati Namba 11 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 11: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri kwani asilimia 47.6 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata zaidi ya alama 7.5 ambazo zilikuwa ufaulu wa wastani. Watahiniwa wenye ufaulu mzuri (21.6%) walieleza aina kuu nne za Shirk na walionesha madhara matatu ya Shirk kwa mujibu wa Qur'an. Watahiniwa wenye ufaulu wa wastani (26%) waliweza kueleza aina nne za Shirk lakini walishindwa kutaja madhara ya Shirk hivyo kupata alama za wastani (7.5 hadi 11). Baadhi yao walitaja aina tatu za shirk badala ya nne na madhara pungufu ya matatu. Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 6.1**

6 Shirk ni kinyume cha tawhid yaani
kufanya kitu kiwe kimoja watu humshiriku
Allah (s.w) na masanamu, mitume, malaika
masharifu na viumbe vyake vingine mfano:
Jua na mwezi

Zifuatazo ni aina kuu nne za
Shirki

Shirk katika dhati ya mwenyezimungu
Ni moja kati ya aina kuu nne za shirki
Shirki hii ni kuchukua miungu mingine
mfano washirikina ~~wamebud~~ wamebuni
miungu yao na huswali, huomba na huchinja
kutokana na miungu hiyo. Mfano leo hii
katika jamii yetu hutumia mizimu kwa ajili
ya kupata mvua, mali na watoto

Shirk katika sifa za mwenyezimungu:
kutokana na shirk hii ni kuchukua sifa
zote za Allah (s.w) kumnasibisha nazo
binaadamu mfano wakristo wamechukua
sifa ya uungu na kumsifia nabii Issa (Yesu)
na baadhi ya waislamu huchukua sifa za
Allah (s.w) kuwasifu masharifu mfano ukarimu
upole, na mtoaji riziki zote ni sifa za Allah (s.w)

Shirki katika mamlaka ya mwenyezi
mungu: Allah (s.w) yeye ndiye lahaye linda
Fisha visha na kuhuisha na hakuna binaadamu
yeyote mwenye kuweza kufanya vyote hivyo
Mfano leo hii katika jamii yetu tunaona kwa
watu wakifiwa na baba na mama wengine
hulia na kusema "tutakula nini na nani atatu
linda" wakati Allah (s.w) yeye ndiye mlinzi

6 Shirk katika ~~hukk~~ hukumu za Mwenyezi mungu: Hukumu za mwenyezi mungu mwizi akatwe mkono, mlevi achapwe fimbo na mzinifu mwanandoa apigwe mawe hadi afe na kama sio mwanandoa achapwe fimbo lakini leo hii katika jamii yetu. wezi wanauliwa au wanachomwa moto au hufungwa gerezani na wazinifu na walevi huachiwa huku ni kuenda kinyume na mafundisho ya Allah (S.w).

Yafuatayo ni madhara ya shirk

Mtu kufutiwa mema yake: Ni kabisa ukimshirikisha Allah (S.w) una futiwa mema yako yote uliyo yatenda nyuma hata kama shirki hiyo ni ndogo ya aina gani

Mja kutosamehewa kosa hilo: Ni kweli kabisa makosa yote utasamehewa lakini kosa la kumshirikisha Allah (s.w) halisamehewi kamwe hata liwe dogo vipi

Mja kuhilikishwa duniani na akhera: Ni kweli kabisa mshirikina hana mafikio yoyote yale isipo kuwa motoni hapia mshirikina ~~huu~~ huwa masikini daima hii inatokana na kutumia mali zao nyingi katika mshirikisha Allah (s.w) mfano kuchinja

Ni kweli kabisa shirki ndiyo sababu itakayo tufanya tuingie motoni na wakati ukiangalia tumetumia mali zetu wenyewe, hivyo watu hatuna budi kumtegemea Allah (S.w) kwa kila jambo li tuwe wenye kufaulu duniani na Akhera

Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza aina kuu nne za Shirk na pia alionesha madhara matatu ya Shirki kwa mujibu wa Qur'an.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa (46.8%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi hivyo kupata alama za chini. Watahiniwa hao waliweza kubaini aina za Shirk ambazo ni sahihi lakini walichanganya

katika kueleza maana ya kila Shirk na pia hawakuweza kuonesha mifano sahihi kwa kila aina ya Shirk. Pia kuna watahiniwa wachache (5.6%) ambao walionekana kutokuwa na uelewa wa mada ya Shirk na maana ya Shirk kwa ujumla hivyo kupata alama 0. Watahiniwa hao walieleza aina za Shirki ambazo sio sahihi kama vile Shirk ya kifo, Shirk ya mizimu, Shirk ya unafiki na Shirk ya uchawi. Wapo pia watahiniwa walioeleza maana ya Shirk kuwa ni kuhudhuria katika sherehe au shughuli yoyote ya pamoja na kufikiri kuwa Shirk ni kitu kizuri sana. Kielelezo 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana ya Shirk hivyo kujibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 6.2**

| | |
|---|---|
| 06 A | - Kushiriki ni kitendo kizuri sana katika m |
| | ujibu wa Qur an katika uislamu watu tunata |
| | kiwa kushilikiana katika jambo mfano mmo |
| | ja wetu amepata tatizo ni mujibu kushiriki i |
| | awere kupona |
| | - Kushiriki ni kitendo kizuri sana kwa sa |
| | babu ~~kesho~~ leo ni wewe kesho ni zamu ya |
| | ko basi unaambiwa utoa ulichonacho kuto |
| | kana na uwezo wako |
| | - Kushiriki ni kitendo kizuri kwa sababu u |
| | nawezo ukapata matatizo mfano msiba |
| | ajari na nyingine huna wa kusaidia lakini |
| | kama wewe ulikuwa unawasaidia wenzio |
| | lazima na wewe usaidiwe |
| | - Kushiriki ni kuzuri unaweza ukaona fed |
| | ha kwa wakati huohuo wakati ulikuwa huna |
| | hata ya hudama ukashangaa fasta unale |
| | tewa mchango kutoka kwa watu wengine |

na kushiriki ni vizuri sana kwakuwa hujui
utapata shida lini kwa matatizo ya wa
nadamu tunatakiwa tushirikiane tutafan
ikiwa katika maisha yetu.

Madhara matatu ya kutoshiriki ku
a mujiwa Qur-an.
- Usiposhirikiana nawenzio ~~mfano~~ kwen
ye shuhulimbalimbali mfano- msiba, harus
i, ajari basi wewe ukatapate tatizo hawata
kusaidia kwa sababu hujawahi kushiriki na
wenzako hata siku moja katika shuhuri hu
wezi kusaidiwa
- Usiposhirikiana siyo vizuri kwasababu hu
takuwa na hela siku ya tatizo lako watoto
matajiri huna utabaki nakusikia aibu mbe
le zawanzako waliokuja kwenye shuhuri
hiyo kubaki kungaa macho tu huna moja
wala mbili.
- Usiposhiriki pia utakosa vifaa vya shi
rika vinavyozunguka kushirikiana mfano
sahani, vikombe, masufuria, navinginevyo ku
wakuwa hushiriki na wenzio utavipata wap
i kila mtu atasema muacheni akome yeye si
hashiriki kwa wenzio atie adabu kwanzaka
ahiyo ndugu waislamu kushirikiane tutap
ata manufaa mbele ya mwenyezimungu na
pia kwa wenzio wanadamu kwaneemazao
kutoka kwa m/mungu watakusaidia.

Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza umuhimu wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za watu badala ya kueleza aina kuu nne za Shirk na kuonesha madhara yake kwa mujibu wa Qur'an.

### 2.2.7 Swali la 7: Kusimamisha Swala

Swali lilihusu mada ya kusimamisha Swala na lilimtaka mtahiniwa kuainisha idadi ya rakaa za swala tano za kila siku kisha kuchambua umuhimu wa kusimamisha swala kwa kutoa hoja sita.

Swali lilijibiwa na Asilimia 43.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 41.1 walipata alama 11.5 hadi 25, asilimia 30.2 walipata alama 7.5 hadi 11 na asilimia 28.7 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 2.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Chati Namba 12 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 12: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi uliofanywa katika majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri kwani asilimia 71.3 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata kuanzia alama 7.5 ambazo ndizo zinazoonesha ufaulu wa wastani kwa swali hili. Baadhi ya watahiniwa (41.1%) waliainisha vizuri rakaa za Swala zote tano na walimudu kuchambua umuhimu wa

kusimamisha Swala. Dondoo zilizotolewa na watahilniwa wengi ni pamoja na Kusimamisha Swala humuepusha mja na mambo maovu na machafu, Swala ikisimamishwa itakuwa sababu ya mja kufaulu na hivyo kuingizwa peponi na Swala ni nguzo ya pili ya uislamu. Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 7.1**


7. Sala ni maombi maalumu ya mja kwa mola wake yanayoanza kwa takbira na kumalizika kwa kutoa salamu. Sala za faradhi kwa muislamu ni tano ambazo zina jumla ya rakaa 17. Sala ya alfajiri ina rakaa 2, adhuhuri rakaa 4, alasiri rakaa 4, magharibi rakaa 3 na sala ya Isha rakaa 4. Hoja zifuatazo zinaonyesha umuhimu wa kusimamisha sala katika Uislamu.

Kwanza, Sala ni amri ya Allah. Allah (SW) ameamrisha na kufadhisha suala kwa kila muislamu mwanamke na mwanamme Allah (SW) anasema katika Qur-ani. "Waambie waja wangu walioamini wasimamis sala". Hivyo mtu anaesimamisha sala huwa anapata radhi za Allah kwa kutii amri y

Pili, Sala ni nguzo ya pili ya Uislamu. Ibn Umar (RA) anasimulia kuwa amemsikia Mtume (SAW) akisema: "Umejengwa Uislamu katika nguzo tano: kutoa shahada mbili, kusimamisha sala ....". Hii inathibitisha kuwa suala ni muhimu kwa muislamu kutokana na kuwa ni nguzo ya Uislamu.

Tatu, Sala humkataza anaesali na mambo machafu na maovu. Nafasi au umuhimu wa kusimamisha sala katika Uislamu ni pamoja na kuwa sala humkataza muislamu na mambo maovu na machafu. Kumkataza muislamu na mambo maovu na machafu ndio lengo kuu la sala kama Allah anavyothibitish

-7- "Hakika ya sala kumkataza (anaesali) na mambo mauvu na machafu."

Nne, Sala ni kitambulisho cha Uislamu

Umuhimu mwengine wa sala katika uislamu ni kuwa sala ndio kitambulisho cha uislamu. Mtume (SAW) anasema "Tofauti (utofauti) kati yetu na hao (wasiokuwa waislamu) ni sala. Na atakaeiacha basi amekufuru. Hivyo ili mtume atambulike kuwa ni muislamu lazima asimamishe sala

Tano, Sala humhakikishia maisha mazuri ya akhera yule anaesali. Miongoni mwa sifa ambazo Allah (SW) amewasifu watu wema katika Qur-ani ni kusimamisha sala. Allah S.W anasema. "Wamefaulu waumini. Ambao ni wanyenyekevu katika sala zao. (13:1-9).

Sita Sala humhakikishia maisha mabaya ya moto kwa anaeipuuza. Pia Allah anasema kuwa atawaathibu wale wote wanaopuuza sala katika Suratul-Maauni "Adhabu kali itawathibitikia wanaosala. ambao sala zao wanazipuuza.

Kwa ujumla sala imechukua nafasi kubwa katika uislamu na hivyo ina umuhimu mkubwa kwa waislamu kwani lengo hasa la swala ni kumkataza na mambo mauvu na machafu yule anaesali. Pia kufutiwa dhambi pamoja na kurehemewa na M-Mungu ni miongoni mwa matunda ya kusimamisha sala."

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeainisha kwa usahihi idadi ya rakaa za swala tano za kila siku kisha kuchambua umuhimu wa kusimamisha swala katika Uislamu.

Hata hivyo, kulikuwa na watahiniwa (26.6%) ambao walishindwa kujibu swali kwa usahihi hivyo kupata alama chini ya wastani. Katika kipengele cha kwanza cha swali baadhi yao badala ya kuainisha kila Swala na rakaa zake walitaja jumla ya

rakaa za Swala za faradhi kwa siku ambazo ni kumi na saba. Katika kipengele cha pili cha swali baadhi yao walitumia mifano kama ndio hoja muhimu za kusimamisha Swala. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa Swala ni muhimu kwani humuepusha mja na zinaa, ushirikina, husda na majivuno, vilevile hujenga umoja, ushirikiano na heshima kwa viongozi. Mtahiniwa alifanya uchambuzi wa hoja moja tu katika maelezo hayo ya swala humuepusha mja na maovu na machafu. Uwasilishaji huu wa majibu kwa kuandika hoja pungufu uliwafanya watahiniwa hao kupata alama za chini. Pia kuna watahiniwa wachache (2.1%) ambao walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kuleta majibu yasiyo sahihi na kupata alama 0. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa istilahi ya "kusimamisha Swala" na kuitafsiri kama kuacha swala na matokeo yake walieleza sababu au udhuru wa muislamu kuacha Swala. Kielelezo 7.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matakwa ya swali.

**Kielelezo 7.2**

| | |
|---|---|
| 7. | Swala - Ni kitendo cha Mwanadamu ~~kums~~ kutubu |
| | na kukiri Maovu yake yote aliyoyatenda na kuswali |
| | ili kutubu Maovu yake yote. Zifuatazo ni idadi ya |
| | rakaa katika swala tano za kila siku ni Asubuhi, |
| | Adhuri, Alasiri, Inshaan na Maghaibi. |
| | Kusimamisha swala kuna madhara mengi |
| | sana na tena ni Makubwa. Kusimamisha swala |
| | kuna Makosa Makubwa na tena ni kosa la jinai |
| | kusimamisha swala watu huwa hawasimamishi swala |
| | ~~kwa~~ bila ya sababu maalumu na ni dhambi kubwa |
| | Kama mtu anasimamisha swala anatakiwa kuwa na sababu |
| | Maalumu. |
| | Kama una Maradhi ya kudumu, Mtu mwenye |
| | Maradhi au ambaye anaumwa anatakia kusimamisha |
| | swala ndo ambapo mtu anatakiwa kusimamisha swala |
| | pale ndipo mtu anapotakiwa kusimamisha swala. |
| | Kma upo kwenye siku. Pale ndipo mtu anapo |
| | ruhusiwa kusimamisha swala ambapo yupo kwenye - |
| | siku za hatari. Hata kama akiswali anakuwa hana - |


7 udhu kabisa.

Kama ni mjamzito: Mtu kama ni mjamzito ndio anaporuhusiwa kusimamisha swala. Maana mtu anapokuwa mjamzito anakuwa hawezi kuswali maana anakuwa hajiwezi kabisa.

Mtu anaetakiwa kusimamisha swala ni mtu aliye jifungua: Mtu aliyejifungua ni Mama ambae hatakiwi kuswali kwasababu anakuwa hana udhu wa kuswali wala kuingia Msikitini.

Unapoacha kwenda Msikitini Ijumaa: Kutokuacha kwenda Msikitini siku ya Ijumaa ni siku ambayo ina baraka na pepo zake zote ambapo Malaika wanapa ba baraka zake zote. Siku ya Ijumaa ni siku ya pepo duniani.

Mtu ambae anatakiwa kusimamisha swala ni mtu ambaye ni kikongwe kabisa ambaye hawezi kuim ama wa kusimamisha swala.

Kwa kuhitimisha: Kuainisha idadi ya rakaa katika swala tano na umuhimu wa kusimamisha swala

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa istilahi ya “kusimamisha Swala” na kuitafsiri kama kuacha Swala na kueleza sababu au udhuru wa muislamu kuacha swala badala ya kuchambua umuhimu wa kusimamisha swala katika Uislamu.

### 2.2.8 Swali la 8: Familia ya Kiislamu

Swali lilihusu mada ya Ndoa katika Uislamu na lilimtaka mtahiniwa kufafanua mambo sita ambayo ni wajibu kwa mume kumfanyia mkewe.

Swali lilijibiwa na Asilimia 46.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 21.8 walipata alama 11.5 hadi 24, asilimia 33.6 walipata alama 7.5 hadi 11 na asilimia 44.6 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 0.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Chati Namba 13 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 13: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Ufaulu wa watahiniwa kwenye swali hili ni mzuri ambapo asilimia 55.4 ya watahiniwa waliofanya swali walipata kuanzia alama 7.5 ambazo zilikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Watahiniwa wengi (21.8%) walikuwa na maarifa ya kutosha ya mada ya Ndoa katika Uislamu hivyo kufafanua mambo ambayo ni wajibu kwa mume kumfanyia mkewe. Baadhi ya watahiniwa walipata alama za wastani (11.5 hadi 15) kwa kuwa walifafanua mambo manne badala ya sita yaliyohitajika. Mambo hayo ni; Mume amtimizie mke wake mahitaji ya lazima; Mume ampende mkewe; Mume atunze siri za nyumbani na Suala la uadilifu. Pia kulikuwa na watahiniwa walioweza kutaja na kueleza mambo sita ambayo ni wajibu kwa mume kumfanyia mkewe. Vile vile watahiniwa hao waliweza kuandika utangulizi na hitimisho zuri hivyo nakupata alama zaidi ya 20. Kielelezo 8.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 8.1**

8 ~~10~~ Ndoa ya kiislamu. Ni mkataba (ngd)
wa hiyari kati ya mkena mume wa kuishi pamoja
kwa wema na upendo kupuatana na masharti na tar
atibu zilizowekwa na sheria ya kiislamu. Zipo
ahazo ni hojo ~~zinazosibitsha~~ ambazo ni wajibu w
a mume kumpanyia mkewe.
Kumvisha, kumnda, na kumpatia ~~mad~~ ch
akula, malazi kwa kadri ya uwezo wake. Kat
ika ndoa ya kiislamu mume anayeoa anala
kiwa apaye mambo muhimu sana kwa mkewe
kwa mpano kumvisha, kumuvisha, malazi na mahita
ji mengine mengi ambayo mume analetawa kuyapa
nye kwa mkewe
Kumtendea wema, kumuhurumia na kumpe
nda. pia katika ndoa ya kiislamu mume anatak
iwa kumpanyia mkewe kumpenda, kumtendea wema
na hata kumuhurumia kwa sababu mke ndiyo a
nayepanya kazi nyingi sana katika ndoa. Hivyo mu
me anapaswa ~~Ndoa~~ kumpenda, kumuhurumia, na kumtend
ea wema mkewe.
Kujizuia na kumchukia mkewe. katika
uislamu pia katika ndoa mume anatakiwa kuji
zuia na kumchukia kwa sababu yeye ni binad
amu anahitaji haki ya kusamehewa kwa kila jam
bo ambalo analitenda kama ni bosi kwa mmewe.
Hivyo basi mume anawajibu kwa mkewe kujizuia na
kumchukia
Kujizuia kumpiga au kuwa mkali sana
kwake. Pia katika ndoa ya kiislamu mume anata
kiwa hawe makini katika suala la kumpiga au kuwa
mkali sana kwa mkewe. Hivyo inatakiwa mume kuwa
mpole na muaminifu katika matendo ya mkewe.

Kutunza siri ya nyumba. Katika nd
oa ya Kiislamu mume anawajibu kwa mkewe kut
unza siri ya nyumba kwa sababu kutunza siri ya
nyumba ni chanzo cha maendeleo katika nyumba
Hivyo mume atakuwa kutunza siri ya nyumba ili s
iri isitoke nje ya nyumba
Kuwa muadilifu. Pia katika ndoa y
a Kiislamu ~~ka~~ mume anatakiwa kuwa muadilifu
kwa mkewe ili waishi kwa raha na upendo k
atika maisha yao hivyo basi ni vizuri mume ku
wa muadilifu katika ndoa pia kwa mkewe
Hivyo mume anatakiwakumfanyia mkewe ma
mbo hayo ili wasiwete madhara katika nyumb
a.

Kielelezo 8.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi mambo sita ambayo ni wajibu kwa mume kumfanyia mkewe.

Hata hivyo, watahiniwa (43.6%) walioshindwa kujibu swali hili vizuri na kupata alama za chini, walionesha kuwa na kasoro za aina mbalimbali kama kutoyajua mambo yaliyo wajibu kwa mume kumtimizia mkewe; kushindwa kutoa maelezo yanayoeleweka kwa dondoo sahihi walizomudu kuzibaini; kurudia jambo moja kwa lugha tofauti, mfano mume ampe mkewe mavazi, chakula na makazi kuwa ni dondoo tatu tofauti kumbe ni vipengele vya dondoo moja ya kumpa mke mahitaji ya msingi. Kielelezo 8.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo 8.2**

(a) kwanza mwanamme ni wajib wake kumshughulik
ia mkewe wake kwa sababu allah (s.w.t) ameeleze
ktk Qur-ani owenye wake kwa hiyo anizeni na
owene wake mumewapende wenyewe sikwa
kulazimishwa na mtu.

(b) Mume ni wajibu wake kumshughulikia mke wake
kwani mwanake kama mume wake hamshughulikii
ipasavyo itakuwa Ndoa hiyo ina migogoro yama
isha mwanamme ni vizuri kumshughulikia
mke wake kwa kumvisha ~~kumvisha~~ kum
lisha na yale yote anayo stahiki kumf
anyia

(c) Mume ni wawajib kumshughulikia mkewa
kwa yale yote anayo yahitaji ktk maisha yao
Ndoa hiyo itadumu na itapendeza ktk
mtazamo wa wanatu wakao itazama Nd
oa hiyo itakuwa allah ameiridhia na ameif
rahia ipasavyo pale mwanamke anayo-
hitaji kitu kwa mume wake mume a
kampatia kile anacho kihitaji

(d) Mume anatakiwa amshughulikie mume wake kwa
sago vile anavyo hitaji kugamiwa na mum
e wake na kumsaidia kazi zake kama
vile mume anastahiki kumfulia mkewe
kumuoshea vyombo kupika n.k.

(e) Ni vizuri zaidi mume kumfanyia mkewa
ke kwa kila ambacho ana kihitajia na m
wanamke nae pia ni vizuri kumfanyia mum
e wake kile ambacho ana kihitaji mu
me atamfurahia mwanamke hiyo na ku
mtekelezea kwa kila ambacho allah ame
mwamrisha mwanamme hiyo kumfanyia m
ke wake na Ndoa.

Kielelezo 8.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeeleza vitu mbalimbali ambavyo mume anapaswa kumnunulia mkewe badala ya kufafanua kwa usahihi mambo sita ambayo ni wajibu kwa mume kumfanyia mkewe.

### 2.2.9 Swali la 9: Ndoa na Talaka

Mada iliyotahiniwa katika swali hili ni Ndoa katika Uislamu. Mtahiniwa alitakiwa kutoa ufafanuzi wa talaka tano zisizorejea. Swali halikufanywa na watahiniwa wengi. Wengi wa waliolifanya swali hili wameonesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya talaka kwani ufaulu wao ulikuwa dhaifu.

Swali lilijibiwa na asilimia 9.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 62.8 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 27.9 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0. Asilimia 18.2 walipata alama 7.5 hadi 11, asilimia 19 walipata alama 11.5 hadi 23 kati ya alama 25. Chati Namba 14 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 14: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache sana kati ya wale waliofanya mtihani huu ambapo ufaulu wa watahiniwa hao ulikuwa wa wastani. Watahiniwa waliokuwa na ufaulu wa chini (34.9%) waliweza kuziainisha talaka zote zisizorejea lakini walizipa maana tofauti, hivyo kuchanganya maana ya talaka hizo. Pia baadhi ya watahiniwa (27.9%) walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kupata alama 0. Watahiniwa hao walieleza nguzo za ndoa ya Kiislamu badala ya kueleza masharti sita yanayopaswa kutekelezwa na muolewaji katika ndoa ya

Kiislamu. Kielelezo 9.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 9.1**

9 Kuna aina kuu mbili za talaka, talaka rejea na
Talaka Isiyo rejea.
Talaka - Ni mfumo ambao umewekwa
katika mwongozo wa kiislamu ambayo mtu ambaye
yeye kawa anapewa kwa namba yakuachwa na mu
mewe. Natalaka rejea ni talaka ambayo mtalaka
wa mara ambayo mwana mke anapaswa kurudi
kwa mumewe mpaka tuwe tayari. Natalaka isiyo
Rejea ni ile talaka ambayo mke ataisha pewa hai
tuhusiwi tena kurudi au kukaa kwa mumew
e labda aolewe tena na ataisho achwa ndipo ata
ruhusiwa aolewe tena na mumewe
Utatamka kwa mdomo: Utatamka kwa mdo
mo. Na kumwambia mke kuwa hauwi tayari na
kutimiza hukumu utaisema zaidi ya mara tatu basi
itakuwa talaka yako imepokelewa na mwenyezi
Mungu na huyo atakuwa si mke tena mpaka
Aolewana achwe ndipo umuoe upya tena
Utaandika: Utaandika kwa mdomo au
Mkono yako kwa kutumia karatasi na peni tala
ka tatu basi huyo si mke tena wa halali ila
Atakuwa wa zinaa. Basi inapaswa umuoe
tena
Utamtumia mjumbe: Kama utamtumia m
jumbe kumuagiza basi talaka yako itakuwa
ime swihi. Hivyo basi huyo siyo mke wako
tena itakubidi umuoe tena na endapo yule
Mwana mke ataolewa na kuachwa na bila ku
Olewa tena hapaswi kumuoa. Ila baada ya ku
Olewa na kuachwa basi mpaka aache
e ndiyo umuoe ili awe wako. Na mwenyezi
Mungu amesema kuipa talaka ndoa hiyo.



| | |
|---|---|
| 9 | kinafsi: Ukimwacha mkeo hatakama |
| | ulikuwa unaongea kinafsi. Basi mwenyezi |
| | Mungu atakuachia hiyo yako na [illegible] |
| ' | Hivyo utakuwa unarudi na huyo mwanamke |

Kielelezo 9.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeeleza aina nne za talaka za kutamka kwa mdomo, kuandika, kumtuma mshenga na talaka za kinafsi ambazo hazipo katika aina za zisizorejewa.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wachache (19%) walikuwa na maarifa ya kutosha ya kuweza kujibu swali hili na kupata ufaulu mzuri. Baadhi ya watahiniwa hao walionesha kuzifahamu vizuri talaka zisizorejea na waliweza kuzitaja aina zake mbalimbali na kutoa ufafanuzi mzuri kwa kubainisha maana ya aina za talaka waliyoitaja na hivyo kupata alama za kuridhisha. Aidha watahiniwa wengine waliweza kufafanua zaidi namna inavyotokea na kisha kuonesha nini cha kufanya endapo mume na mke wanataka kurudiana. Aina za talaka zisizorejewa ni pamoja na Talaka tatu, talaka ya I'laa, talaka ya Zihar, talaka ya Li'an na talaka ya Khul'u. Watahiniwa hao walipata alama nzuri. Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi.

**Kielelezo 9.2**

9: Talaka ni kuvunja mkataba wa kindoa baina ya mke na mume kwa kuto ishi kwa pamoja. Kuna aina mbili za talaka katika Uislamu Talaka rejea na isiyorejea. Zifuatazo ni aina za talaka zisizo rejea

Talaka Ilaa: Hii ni aina ya talaka isiyorejea ambayo hutokea pindi mtu akamua kujitenga na mkewe kwa zaidi ya miezi minne (4) Baada ya muda huo kupita basi ndoa hiyo huvunjika na mke yule si mke tena halali wa mume yule na mume kama anamtaka mkewe kumrejea basi atafunga nae ndoa upya kwa mahari mapya.

Talaka Khul-u: Pia talaka khul-u ni aina ya talaka isiyorejea inatokezea pale pindi mke atakapodai kuachwa na mumewe kwa vile hapati fursa ya kufanya mambo yake anayoyataka, na hapati amani katika ndoa na iwapo mumu hakum yima haki yoyote katika haki zake bilafsi mke atalazimika kurejesha mahari ya mume

Talaka Zihaar: Talaka zihar hutokezea pale mume atakapo susa na mkewe na mume kum wambia mkewe "nakuona kama mgongo wa mama yangu" basi hapo mke kachaashuka na kafara yake ni kumwachia huru mtumwa au kufunga miezi miwili (2) mfululizo au kuwalisha maskini sitini (60) kabla ya miezi nane kumalizika

Talaka tatu: Talaka tatu pia ni aina ya talaka isiyorejea hii hutokezea pale mume atakapo muacha mkewe talaka zote tatu. na mume haruhusiki kumuowa mke yule tena mpaka katika kipindi cha eda mpaka aweze kuolewa na kuachwa kwa mume mwengine ndio anaru

husika kumuoa tena mke yule kwa mahari mapya.

Talaka ya Lian: ni aina ya talaka isiyorejea ambayo hutokezea pale mume kumsingizia mkewe suala la zinaa kwa kula viapo vinne mke huyo Itakuwa Kashaachika na mume yule

kwa hiyo: Katika Uislam suala la talaka si Suala la kufanyia mashara mume anapo~~muacha~~ ~~Mke~~ kaa na mke wake akae nae kwa kumpenda na kumuheshimu bila ya kumfanyia hitilafu ya aina yoyote ile katika ndoa ili isiweze kufikia Suala la talaka

Kielelezo 9.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyetaja na kueleza kwa usahihi aina za talaka zisizorejea ambazo hazipo katika daraja ya zisizorejewa.

## 2.2.10 Swali la 10: Vita vya Uhud

Swali lilihusu mada ya Upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu na lilipima ufahamu wa watahiniwa juu ya vita vya Uhud. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua mafunzo sita yatokanayo na vita vya pili vikubwa alivyoshiriki Mtume (s.a.w.).

Swali lilijibiwa na asilimia 48.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 71.2 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 16.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 19.6 walipata alama 7.5 hadi 11, asilimia 9.2 walipata alama 11.5 hadi 23.5. Chati Namba 15 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 15: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni hafifu. Hii inatokana na ukweli kuwa asilimia 71.2 ya watahiniwa wote walipata chini ya alama 7.5 ambao ndio ulikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Watahiniwa waliopata alama za wastani (19.6%) hawakuwa na maarifa ya kujibu swali kwa usahihi. Watahiniwa hao walichanganya mafunzo sahihi ya vita vya Uhuud na mafunzo yasiyo sahihi. Pia watahiniwa hao hawakuwa na melezo ya kina pamoja na mifano juu ya mafunzo waliyoyaainisha na wengine waliainisha mafunzo ya aina moja kwa maneno tofauti. Kwa mfano walieleza mafunzo ya umuhimu wa kumtii Mtume, kumheshimu Mtume na kumfuata Mtume kuwa ni mafunzo tofauti. Vilevile watahiniwa wengine (16.2%) walishindwa kutambua vita vya pili alivyoshiriki Mtume (s.aw) na hivyo kujibu kinyume na maelekezo ya swali na kupata alama 0. Badala ya kuchambua mafunzo ya vita vya Uhud ambavyo vilikuwa vya pili, watahiniwa hao walichambua mafunzo ya vita tofauti tofauti kama vile vita vya Badri, Handak na Ahzaab. Kielelezo 10.1 kianonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.

**Kielelezo 10.1**

| | |
|---|---|
| 10 | Vita vya pili Vikuubwa alivyoshiri |
| | ki mtume ~~ta~~ (S.a.w) katika kulinga |
| | nia dini ya mwenyezi mungu (allah) v |
| | ilitusaidia katika kupata mafunzo mb |
| | alimbali kama ifuatavyo. |
| | Kuamini Uwepo wa ALLah, Hak |
| | ika katika vita hii watu waliamini |
| | uwepo wa mwenyezi mungu (ALLah) h |
| | a baadhi ya watu kusilimu (kubadi |
| | li dini au mwelekeo wao na kurud |
| | ia kwa allah., hali hii pia ilisai |
| | dia watu kuamini katika Imani ili |
| | yoimara |
| | Kuamini Uwezo wa mtume, baad |
| | hi ya watu walimdharau mtume pa |
| | moja na wafuasi wake bila kujua k |
| | wake mtume alipewa nafasi ile kwa |
| | Uwezo wa allah na ilimsaidia mtu- |
| | me kushinda katika Vita vile ndipo |
| | watu wakamuamini mtume na kum |
| | Sujudia hakika yeye ni mjumbe wa mw |
| | enyezi mungu (allah) |
| | kuamini Siku ya mwisho, hak |
| | ika baadhi ya watu walikuwa ha |
| | wa amini Uwepo wa Siku ya mw |

10 mwisho ndani ya Vita ile ilisaidia
watu kuamini na pia watu kul
udi kwa mwenyezi mungu <allah>
kwa kuomba msamaha na kumuabudu
mwenyezi mungu maana vita ile ilik
uwa mfano wa Siku hiyo ambapo k
ila aliyengiambo ya bahari atamuon
a ~~mwenze~~ mwenzie hii ndio imani
na mafunzo tuliyoyapata katika V
ita hii.
Kuamini siku ya malipo, Mwenye
zi mungu <allah> ameahidi kutoa m
alipo kwa aliyedhulumia. na pia kat
ika Vita hiyo mwenyezi mungu ali
onyesha kuwa katakuwa na Siku
ya malipo mfano katika kisa cha
firauni ambaye alijiita mungu baad
a ya kufa kwake mbingu na ardhi
vilimkataa na watu kumuweka kam
a makumbusho katika mji wa misri
hali hii inatuonyesha jinsi mwenyezi
mungu alivyokuwa na uwezo na pia
baadhi ya malipo hulipwa hapa ha
pa duniani hata hivyo vita hii ilis
aidia watu kumuamini mwenyezi
mungu na mitume wake na kuwa
yeye ndiye mpangaji na ndiye mtoaji
wa kila kitu hapa duniani na k
esho ahela na baadhi ya watu ku
wa na Imani Hata hivyo watu kutokuami
ni ~~tt~~ uwepo wa mwenyezi mungu n
a ~~kut~~ kwenda kinyume na maam

10 nsho yake na Sheria za kidini zina vyosema.

Kuamini Vitabu, katika Imani zetu Inatupasa kuamini Vitabu vya muenyezi mungu <Qur'an> katika Vita ile baadhi yao walidhani kuwa Qur'an imetoka Arabic ambapo Lugha wanayoitumia ni kiarabu Katika Imani za kidini Inatupasa Kuamini katika Imani za kidini <Uislamu>

Kuamini malaika, Inatupasa kuwaamini malaika wa mwenyezi mungu kwa ndio ambao hutufikishia Ujumbe kwa njia ya ndoto hata hivyo katika Vita Ili baadhi ya watu walipata kuwaamini malaika wa mwenyezi mungu <Allah>

Hata hivyo baadhi ya watu bado hawaamini kuwepo kwa mwenyezi mungu <Allah> na kushindwa kusimama katika vyo vya Imani dhabiti pia baadhi ya mafunzo ya dini Vitoe mafunzo juu ya Imani iliyodhabiti ambayo Imani hiyo ndiyo itakayowapeleka watu mahali pazuri napatakafufu <peponi> haya ndiyo mafunzo tuliyoyapata baada ya mtume (s.a.w) kushiriki katika Vita vya pili vikubwa.

Kielelezo 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza nguzo za imani ya Kiislamu badala ya kuchambua mafunzo sita yatokanayo na vita vya pili vikubwa alivyoshiriki Mtume (s.a.w.).

Watahiniwa wachache (9.3%) waliweza kujibu swali hili na kupata alama za juu. Baadhi ya watahiniwa hao walitambua kuwa vita vya pili vilivyokusudiwa kwenye swali ni vya Uhud na hivyo kuyabaini mafunzo na kutoa maelezo ya kuhusu mafunzo hayo. Hata hivyo, watahiniwa hao walibainisha mafunzo pungufu ya sita hivyo kupata alama za kati (11.5 hadi 17). Watahiniwa wengine waliweza kubaini mafunzo sita ya vita vya Uhud na kutoa maelezo ya kina pamoja na utangulizi na hitimisho zuri hivyo kupata kuanzia alama 18 hadi 23.5. Mafunzo yaliyotolewa na watahiniwa hao ni pamoja na Waislamu kujizatiti kwa kadri ya uwezo wao katika kupigania dini ya Allah (s.w), kutovunja amri ya Allah (s.w) na mtume wake, kutoyafumbia macho makosa ya watu wachache kwani athari ikitokea itakuwa kwa jamii nzima, kuliwazwa waislamu kwa kutangaziwa msamaha baada ya kurejea katika mapambano na njia pekee ya kuwabainisha wanafiki katika jamii ya waislamu ni kupigania dini ya Allah (s.w). Kielelezo 10.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 10.2**

| | |
|---|---|
| 10. | Vito Vya pili Vikubwa aliyo shiriki bwana |
| | Mtume Swala Llahu Alaihi Wassalam vilikuwa- |
| | ni Vita Vya Uhudi. Sababu ya kuitwa vita |
| | hivyo "UHUD" ni kwa Sababu Vilipiganwa ka- |
| | tika mlima wa Uhudi. Sababu ya Vita hivyo |
| | ni kutaka kulipiza kisasi makurashi kwa |
| | waislam, hivyo wakajipanga upya. Kwa kupitia |
| | Vita hivyo tuna pata mafunzo mbali mbali. |
| | Yafuatayo ni mafunzo tunayo yapata |
| - | kutoka katika Vita vya Uhud. |
| | Kufuata amri ya Mtume ni Muhimu; Katika |
| | mafunzo makubwa tunayo ya pata katika |
| | Vita hivyo tunao kuwa Sababu ya kushindwa |
| | kwa waislamu ili kuwa ni kuvunja amri ya |
| | mtume baada ya kushuka juu ya mlima |
| | walioambiwa wasishuke mpaka amri ya |
| | mtume, baada kuona makafiri wana kimbia |
| | walishuka, hatimae wakageukiwa, laiti wasingeli |
| | khalifu wasingelishindwa. |
| | Ushindi Unatokana na Allah; Pia kwa |
| | kupitia matukio yaliyo jitokeza katika Vita |
| | hivyo tunajifunza kuwa Allah pekee ndiye |
| | anayo toa Ushindi pale apendapo, kwa Sa- |
| | babu waislamu walikuwa wakiamini kuwa- |
| | mba watashinda kutokana na Wingi wao pamoja |

10 Maandalizi ya kutosha lakini matokeo yake ilitoke kile ambacho hawa kukitegemea katika fikra zao. hivyo basi wategemewa ni Allah pekee si wingi wa watu au majeshi au Ubora wa silaha/zilizo bora.

Vita Vinaitaji Mipango na Maarifa: Pia Kutokana na matukio ya Vita hivi ya Uhud tunapata kujifunza kwamba Vitani mipango na maarifa kwa sababu tunaona ni jinsi gani ambavyo Bwana Mtume alivyotumia maarifa na akili ya kuwa pandisha watu milimani na pia Vile vile Khalid ibn Walied alivyotumia maarifa ya kuwazunguka waislamu na hatimae walijweza kushinda jeshi kubwa la waislamu.

Mali ni Mtihani duniani: Miongoni mwa matukio yaliyotokea katika Vita hivi ya Uhud tunapata kujifunza kuwa mali ni mtihani duniani kwa Sababu Chanzo cha watu waliamrishwa kulinda pande za milimani ~~na kwa~~ sababu kubwa iliyowapelekea kushuka ni kuwania mali au ngawira baada ya kuona makafiri wanakimbia na kuacha mali mbali mbali, hatimae walirungukiwa kwa nyuma na kushindwa.

Makafiri Siku zote wana Uwadui na Uislamu: Pia tunajifunza ~~kwamba~~ kutokana na Vita hivi ya Uhud kuwa mbu siku zote makafiri hawana Urafiki bali ni maadui milele Zidi ya Uislam na waislam, kwa sababu baada ya kushindwa Vita ya nyuma au

| | |
|---|---|
| 10 | vya kwanza vya badri hawakukata tama |
| | a na kuacha Uislamu bali walijipanga |
| | upya kupotea na kuidirisha mira Uislamu |
| | kwa njia Vita Vingine ambavyo ndivo Vita |
| | vya Uhudi |
| | Kosa la wachache linaweza likaathiri |
| | Umma; Pia tunaona kwamba tunaweza |
| | kujifunza kutokana na matukio ya Vita hivi |
| | kuwa Kosa la wachache linaweza kuathiri |
| | Umma. kwa sababu tunaona wali'o khalifu |
| | amri ya mtume wali'kuwa ni wati wachache |
| | wasio ~~punga a to~~ zidi' wati khamsini lakini |
| | baada ya kufanya kosa ili'athiri kundi' lote |
| | la jeshi la waislam. |
| | Hayo ndio mafunzo tunayo yapata kutoka |
| | na na matukio yaliyo tokea kati ka Vita |
| | Vya pili Vikubwa walivyo ~~p~~ shiriki mtume |
| | dhidi ya makafiri, kama tuna vyoona hapo |
| | juu mfuno Umuhimu wa kutii amri ya mtum- |
| | e na Kosa la wachache linaweza kuathiri |
| | Umma mzima na mengineyo. |

Kielelezo 10.2 kinanonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechambua kwa usahihi mafunzo sita yatokanayo na vita vya pili vikubwa alivyoshiriki Mtume (s.a.w.).

### 2.2.11 Swali la 11: Dola ya Kiislamu baada ya Kutawafu Mtume (s.a.w)

Swali lilihusu mada ya historia ya dola ya Kiislamu baada ya kufa Mtume (s.a.w.) na lilimtaka mtahiniwa kueleza njia tatu za kumpata Khalifa kisha kubainisha majukumu manne ya Khalifa kwa kurejea historia ya dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.).

Swali lilijibiwa na asilimia 17.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 77.3 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 15.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 14.6 walipata alama 7.5 hadi 11, asilimia 8.1 walipata alama 11.5 hadi 23.5. Chati Namba 16 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 17: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni hafifu. Hii inatokana na ukweli kuwa asilimia 77.3 ya watahiniwa wote walipata chini ya alama 7.5 ambazo ndio zilikuwa ufaulu wa wastani kwa swali hili. Watahiniwa hao walionekana kutojua njia za kumpata Khalifa kwa kutojua utaratibu uliofuatwa ili kumpata Khalifa baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.). Watahiniwa hao walieleza kuhusu uchaguzi au uteuzi wa viongozi kwa kutumia taratibu zilizozoeleka katika serikali za kidunia kwa kuainisha njia zilizotumika pamoja na kuchaguliwa kwa kura au kuteuliwa au kufanya mapinduzi. Watahiniwa wengine walielezea sifa za mtu anayefaa kuwa Khalifa kama vile awe na umri mkubwa, awe amehifadhi Qur’an na Hadithi za Mtume na awe mcha Mungu. Kwenye majukumu ya Khalifa walitoa maelezo ya jumla kama vile Khalifa analo jukumu la kuwapenda, kuwasikiliza, kuwahurumia waislamu, kuwa mkweli na mwaminifu kwa waislamu. Kielelezo 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 11.1**


11. Dola ya kiislamu; Ni kipindi ambacho
katika upande wa walengwa mtume aliyeanzisha dola-
ya kiislam wakati Sunnah za Maadhehebu zinazohusiana
ama kutolewa katika ulimwengu huu wa sasa. Baina-
sha majukumu ya Khalifa nazo ni kama zifuatazo-

Elimu; katika kipindi cha Dola ya Kiislam
u Khalifa alipewa jukumu la elimu na kuweza
kuwaelimisha watu wengine hapo zamani na
kuweza kuwasaidia watu wengine kielimu hivyo
kumpata Khalifa ilikuwa sawa jambo zito katika-
kuelimisha kwake.

Kutunza Dola ya Kiislamu; kwa kumpata
Khalifa katika Dola ya Kiislamu na kuweza kuitunza
ama kulinda katika dini hii ya Kiislamu na kuweza
kuona na Khalifa kwa wepesi zaidi kwa kuweza
kuiweka hiyo Dola ya kiislamu hapo duniani

Katika kushirikiana na ujenzi wa Kiisla-
mu; Na katika njia nyingine hapo awali kwa
kumpata Khalifa katika ujenzi wa Kiislamu pamoja-
na dola ya kiislamu kwa kuweza kushirikiana
na wenzie hapo enzi ya ukhalifa

Na katika Dola ya Kiislamu lugha iliy
otumika ni ya kisheria na ufafanuzi;
Katika upande wa dola ya kiislamu lugha iliyo-
tumika ni nyepesi na ufafanuzi mzuri inayo
mfundisha ama inayomgusa mtu mwenyewe mhu-
sika pale ambapo atakapotoka nje ya masharti na-
mafunzo yao wao wenyewe ndipo ufafanuzi huo
unaeleweka wenyewe

Mwisho; Haya yote ni historia ya Dola ya
Kiislamu baada ya kutawafu mtume (s.a.w) hadi
Makhalifa wanne waongofu hayo ndiyo yaliyoto-
kea katika Dola ya Kiislamu.

Kielelezo 11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza historia ya dola ya Kiislamu badala ya kueleza njia tatu za kumpata Khalifa na kubainisha majukumu manne ya Khalifa.

Aidha, wapo watahiniwa wachache (8.1%) walioweza kujibu swali hili na kupata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa mada ya historia ya dola ya Kiislamu baada ya kufa

Mtume (s.a.w.) hivyo waliweza kuonesha namna alivyopatikana Khalifa wa kwanza yaani Abubakar (r.a). Pia walizitaja dalili mbalimbali zilizoachwa na Mtume (s.a.w.) zilizowaongoza maswahaba kumteua awe kiongozi wao. Aidha, walionesha alivyopatikana Khalifa wa pili, wa tatu na wa nne. Watahiniwa wengine walimudu pia kuainisha vizuri majukumu ya Khalifa wa Dola ya Kiislamu ambayo ni pamoja na kujenga maisha ya binadamu juu ya msingi wa ucha Mungu na matendo mema, kulinda mipaka ya dola kwa gharama yoyote, kuteua viongozi mbalimbali wa dola ikiwa ni pamoja na wakuu wa majimbo na kusikiliza kesi na kutoa hukumu stahili kwa mujibu wa sheria ya Uislamu. Kielelezo 11.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 11.2**

11\. Dola ya kiislamu ni dola ambayo ameianzisha mwenyewe mtume (SAW) kwa madhumuni ya kuendeleza uislamu baada ya kutawafu mtume (SAW) makhalifa wanne waliongoza dola hiyo makhalifa hao ni Abubakar bin Quhafa, Umar, Uthman bin Affan pamoja na Aliy bin Abi Muttalib. Khalifa ni kiongozi mwanamme aliyechaguliwa kwa lengo la kuendeleza Uislamu kupitia njia mbali mbali kama

Mapendekezo hii ni njia ambayo imetumika katika kumweka madarakani khalifa Abubakar, mapendekezo hayo yalimpendekeza Abubakar kwa sababu alikuwa ndie Imamu kipindi ambacho mtume (SAW) anaumwa. pia alikuwa ni mtu ~~[illegible]~~ mzima wa kwanza kusilimu pia alijua kusoma quran vizuri, ~~[illegible]~~ Abubakar (RA) alitangaziwa mbele ya kamati kuwa khalifa ndipo akapewa (baia) ahadi ya utii.

Kuteuliwa njia hii ilitumika kumweka madarakani Khalifa wa pili Umar, aliteuliwa na Abubakar kutokana na imani yake juu ya uislamu na uchamungu aliokuwa nao, kuteuliwa huko kulingana baadhi ya watu kuogopa uongozi wake kutokana na tabia yake ya ukali aliokuwa nao lakini Abubakar (RA) alimtaja wazi wazi kwa kuwaambia kazi hii ya uongozi itamfaa kuwa mmoja.

Kuchaguliwa pia hii ilitumika katika kumuweka madarakani khalifa wa ~~nne~~ 3 Uthman bin Affan (RA) kuchaguliwa kwako kulitokea watu wengi wenye sifa zilizofanana ndipo Umar (RA) akateua jopo la watu sita na kuwapa siku tatu wawe washachagua khalifa atakaeendeleza kuongoza dola ya kiislamu baada ya mchakato kumalizika. Siku tatu baada ya kufariki Umar (RA) alitangazwa Uthman (RA) kuwa khalifa wa tatu na kupewa ahadi ya utii.

Kutokana na njia hizo pia khalifa anayo majukumu mengi ambayo anatakiwa kuyafanya ili kuendeleza dola ya kiislam nayo ni:

Kuteua wajumbe wa Shura au magavana, jukumu hili khalifa wa 4 Aliy (RA) aliitilia mkazo na kuamua kuchagua magavana 17 ambao alishirikiana nao katika mambo mbalimbali.

Khalifa ana wajibu wa kuwa yeye ndo hakimu au mahakama ambapo akisikia mtu kafanya kosa lolote mfano wizi, mtu kaiba kuku basi wajibu wake kwenda kumuadhibu mtu huyo hata kama yuko nyumbani kwake kwa kumpa adhabu na hukumu aliyoiamrisha Allah (SW) ikiwa hukumu ataitoa peke yake au kushirikiana na wajumbe wake ili kuleta usawa katika jamii.

Kuamrisha mema na kukataza mabaya. Khalifa anao wajibu mkubwa wa kuamrisha jamii kutokana na utendaji mema pamoja na kuifahamisha jamii yao ya kuyaacha mambo mabaya ambayo Allah (SW) ameyakataza mfano wa mambo mema yakuamrisha ni pamoja na Swala, Saka na funga. mfano wa mambo mabaya au maovu ya kukataza ni ulevi, riba na usinifu.

Kushughulikia baitul mal ambayo ni hazina ya waislamu. Khalifa hana budi kuwa ndio kiongozi wa hazina ambayo hukhifadhiwa vitu maalum kama vile Zakat na Sadaqat na kuhakikisha watu wote waliokusudiwa kupatiwa Zakat pamoja na Sadaqat wanapatiwa wenyewe pindi itakapofika wakati wa kugawa kwa watu hao miongoni mwao ni mafukara, maskini watumwa na kuwasaidia watu wenye madeni makubwa katika kulipa madeni hayo.

Kutokana na wajibu wa khalifa mwanadamu pia ni khalifa wa Allah (SW) kwahivyo hana budi kutekeleza sheria wajibu wake wa kumcha Allah (SW) usiku na mchana tukifanya hivyo tutapata kufahamu vizuri wajibu wa kila khalifa hapa duniani.

Kielelezo 11.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi njia tatu za kumpata Khalifa na pia alibainisha majukumu manne ya Khalifa kwa kurejea historia ya dola ya Kiislamu baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.).

### 2.2.12 Swali la 12: Maadui wa Dola ya Kiislamu Madina

Swali lilihusu mada ya upinzani dhidi ya dola ya Kiislamu Madinah na lilipima uelewa wa mtahiniwa katika kueleza mambo sita yanayodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya Dola ya Kiislamu Madinah.

Swali lilijibiwa na asilimia 22.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Asilimia 79.6 walipata alama 0 hadi 7 miongoni mwao asilimia 26.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0, asilimia 13.4 walipata alama 7.5 hadi 11, asilimia 7 walipata alama 11.5 hadi 22.5. Chati Namba 17 inaonesha ufaulu huo kwa asilimia.




Chati Namba 17: Mwonekano wa Alama za Watahiniwa kwa Asilimia

Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni hafifu. Watahiniwa wengi (79.6%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi na kupata chini ya alama 7. Watahiniwa wengi (53%) walieleza uadui wa makafiri kwa ujumla wakijumuisha vitendo vya dunia ya sasa dhidi ya uislamu ikiwemo; waislamu kuitwa magaidi, nchi za waislamu kuvamiwa na Masheikh kufungwa bila sababu. Watahiniwa hao walipata alama za chini kwa sababu majibu yao yalikuwa mafupi na yanayoeleza mambo pungufu ya sita. Watahiniwa (26.6%) waliopata alama 0, walishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kujibu kinyume na walichoulizwa. Wengi wa watahiniwa hao, walijikita katika sifa za wanafiki kama zilivyoelezwa kwenye Hadithi ya mtume inayoeleza sifa tatu za mnafiki ambazo ni kutotimiza ahadi, kusema uongo, kuvuka mipaka pale wanapoaminiwa. Pia walieleza vitimbi vya makafiri dhidi ya Mtume (s.a.w.) na wafuasi wake. Kwa mfano, kuwatukana, kuwaua, kuibeza

Qur'an na kuanzisha vita dhidi ya Waislamu. Wengine walieleza kuwa wanafiki walipinga misingi yote aliyoiasisi Mtume (s.a.w) alipokuwa akiweka misingi ya dola ya Kiislamu hivyo walielezea kuwa wanafiki walikataa ujenzi wa msikiti, upatanishaji wa kabila la Aus na Khazraj, Katiba ya Madinah na uundwaji wa sekretarieti ya Mtume. Majibu yote hayo hayakuwa sahihi na yalisababisha watahiniwa kutopata alama. Kielelezo 12.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 12.1**

12. Dola ya Kiislamu, ni taasisi inayohusiana na mambo ya Kiislamu katika uislamu. Yafuatayo ni mambo yanayodhibirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya Kiislamu Madinah:

Kujengwa kwa msikiti, hili ni jambo linalodhibirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya kiislamu madinah baada ya mtume muhammad (s.a.w) kujenga msikiti madinah.

Kujengwa kwa ummah wa Kiislamu, hili ni jambo linalodhibirisha uadui wa ~~makafiri~~ wanafiki dhidi ya dola ya kiislamu madinah baada ya mtume (s.a.w) kujenga ummah wa Kiislamu madinah.

Kuwekwa kwa mkataba wa amani, hili ni jambo linalodhibirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya Kiislamu madinah baada ya mtume (s.a.w) kuweka mkataba wa amani madinah.

Kuwekwa kwa mkataba wa madinah, hili ni jambo linalodhibirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya kiislamu madinah baada ya mtume kuweka mkataba wa madinah.

Kuimarishwa kwa uchumi, hili ni jambo linalodhibirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya kiislamu madinah baada ya mtume (s.a.w) kuimarisha uchumi madinah ikadhibirisha uadui huo


12. Kuteua sekritari na shura, hili ni jambo linalodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya Kiislamu madinah badala ya mtume (s.a.w) Kuteua sekritari na shura madinah.

Hitimisho, Kutokana na mambo yanayodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya kiislamu madinah, madinah ni sehemu ilizowalenga wanafiki na ujumbe wao ni kujenga dola ya kiislamu.

Kielelezo 12.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeeleza hatua alizozitumia Mtume Muhammad (s.a.w) kuunganisha umma wa Kiislamu badala ya kueleza mambo sita yanayodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya Dola ya Kiislamu Madinah.

Watahiniwa wachache (7%) waliojibu swali hili vizuri waliweza kuainisha mambo mbalimbali yadhihirishayo uadui wa wanafiki dhidi ya Dola ya Kiislamu yakiwemo; kula njama na makafiri kutaka kumdhuru mtume na waislamu, kujiengua kwenye misafara ya vita; kuzua uongo dhidi ya waumini kama kumsingizia Bi Aisha (r.a) kuwa kazini, kuwagombanisha waumini kama kisa cha Aus na Khazraj na kujenga msikiti ili kiwe kichaka cha kuhujumu Uislamu huku wakipanga kumuua Mtume (s.a.w) pindi atakapouzuru msikiti huo. Kielelezo 12.2 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

**Kielelezo 12.2**

12 Katika kuhuisha dola ya Kiislamu mjini Madinah Mtume Muhammad pamoja na maswahaba zake walikuwa na wanafiki miongoni mwa wafuasi wa Mtume ambao walikuwa wakikwamisha baadhi ya mambo katika harakati za kuhuisha dola ya Kiislamu. Miongoni mwa mambo yaliyodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya dola ya Kiislamu ni haya yafuatayo.

Kutoa nyuzuri mbalimbali zisizo za msingi wakati wa kwenda kwenye jihad, Wanafiki walikuwa wakitoa visingizio vya hapa na pale ili wasiweze kwenda kuhudhuria vita au jihad ya Mtume Muhammad (s.a.w) dhidi ya washirikina na Makafiri ambapo baadhi yao walikuwa wakidai kuwa wanaumwa ilimradi wasiende vitani kwa ajili ya kumaumwa, makafiri na washirikina katika mji wa Madinah.

Kumzulia mke wa Mtume kuwa ~~amedh~~ amezini na Swahaba Sufiani, Pia wanafiki walianza kumzulia mke wa Mtume bi Aisha (r.a) kuwa amezini na Swahaba wake ili wapate kumgombanisha Mtume Muhammad na mkewe lakini kutokana na hekima yake ikajabainika kuwa bi Aisha (r.a) alizushiwa na hakuzini. Haya yote yalikuwa ni kutaka kumgombanisha Mtume na ndugu zake pamoja na ndugu wa bi Aisha (r.a).

Kuwagombanisha Ansuar na Khazraj, Wanafiki waliwagombanisha miongoni mwa makabila makubwa kabisa katika mji wa Madinah ambao ni Ansuar na Khazraj ili kutaka kuwasambaratisha waislamu wasiwe wamoja katika kupigania na kusimamisha dola ya Kiislamu katika mji wa Madinah lakini Mtume Muhammad (s.a.w) aliweza kuyapatanisha makabila hayo na hatimaye kuendelea na juhudi zao za kuhuisha uislamu Madinah.

12 Kujenga msikiti kama kituo kikuu cha kupiga-
vita uislamu katika mji wa Madinah, wanafiki wali
amua kuanzisha sehemu ambayo itakuwa rahisi kwa
o kuweza kupiga vita uislamu na kuukakanda-
miza na hivyo kuamua kujenga msikiti ili uwe-
katika sehemu ya mkutano yao katika kupiga
vita uislamu katika mji wa madinah na hivyo kud-
umaza harakati na kusimamisha uislamu.

Kuwa pamoja na makafiri na washirikina kati-
ka njama za kumuua mtume, wanafiki waliung
ana na makafiri na washirikina katika azma-
yao ya kutaka kumuua mtume ili waweze-
kudumaza harakati za kuhuisha uislamu katika-
mji wa Madinah ambapo baadhi ya wanafiki-
walitumika kumchunguza mtume ili wamuue, laki
ni kwa uwezo wa Allah (S.w) hawakufanikiwa-
na harakati hizo ziliendelea kama kawaida.

Kujitenga wanafiki 300 katika vita vya UHUD na
kumwacha mtume Muhammad akiwa na jeshi la wai-
slamu 700 dhidi ya makafiri 3000 ambapo hata-
hivyo waislamu walishinda kutokana na rehma-
ya Allah (S.w) japokuwa waliumia sana, ila wal
e wanafiki 300 wangeongezeka wangeongeza nguvu-
na kupunguza maafa kwa waislamu ambapo wange-
weza kuwakabili makafiri vizuri. Lakini kutokana-
na unafiki wao waliletea madhara kwa waislamu.

Kwa kumalizia, wanafiki ni watu hatari-
sana katika jamii zetu hasa jamii za kiislamu-
kwani huweza kukwamisha maendeleo ya waisla-
mu katika jamii na kuleta madhara makubwa
kwa waislamu kwa ujumla.

Kielelezo 12.1 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeeleza mambo sita yanayodhihirisha uadui wa wanafiki dhidi ya Dola ya Kiislamu Madina.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Tathmini ya karatasi ya kwanza ya mtihani huu inaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada za *Fiqh, Tarekh, Qur'an na sunnah na Hadithi* na walikuwa na ufaulu wa wastani katika mada za *Tawhiid*. Katika karatasi ya pili ufaulu wa watahiniwa ulikuwa ni mzuri katika mada za *Fiqh* na *Tawhiid* na wa wastani katika mada za *Qur'an*. Pia ufaulu hafifu ulionekana katika mada ya *Tarekh*. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika karatasi ya kwanza ni mzuri ukilinganishwa na ufaulu wao katika karatasi ya pili (rejea kimbatisho A).

Sababu za watahiniwa kufanya vibaya ni pamoja na kuandika majibu yasiyoendana na matakwa ya swali, kutosoma na kuelewa vizuri matakwa ya swali na uwezo mdogo wa watahiniwa kueleza dondoo sahihi walizozitaja. Mada iliyofanyika vizuri zaidi ni mada ya *Qur'an* (*Sura Zilizoteuliwa)* ambayo ilikuwa na asilimia 79.1 na mada iliyofanyika vibaya zaidi ni mada ya *Tarekh (Upinzani dhidi ya Dola ya Kiislamu Madina)* ambayo ilikuwa na asilimia 20.4 wakati mada iliyofanyika kwa wastani ilikuwa mada ya Tawhiid (*Kuamini Mitume wa Mwenyezi Mungu)* ambayo ilikuwa na asilimia 40.5. Kwa ujumla ufaulu wa mwaka 2015 umepanda kwa asilimia 24.67 ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2014 (rejea kiambatisho B).

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Mtihani wa Kidato cha Nne katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2015 ulizingatia Muhtasari wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa kilikuwa ni kizuri ambapo wastani wa ufaulu kwasomo hili ni asilimia **51.2**.

Uchambuzi huu ulionesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile kutofuata maelekezo ya swali, kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza na uelewa mdogo wa mada mbalimbali na hasa mada za *Tarekh* na *Tawhiid*. Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu kwa mada zote katika mtihani wa Kidato cha Nne, jitihada zinahitajika katika

ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea watahiniwa ujuzi katika kujieleza bila kikwazo chochote hasa ikizingatiwa kuwa Elimu ya Dini ni msingi mzuri kwa kumuandaa mtoto kimaadili.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa wajao wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mambo yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Ni muhimu walimu wajitahidi kufundisha na kumaliza mapema mada zote za muhtasari ili kuwapa fursa watahiniwa kufanya rejea mbalimbali katika kujiandaa na mtihani.

(b) Watahiniwa wajengewe tabia ya kujisomea vitabu vya kiada na ziada ili kuimarisha maarifa wanayoyapata darasani na waweze kutoa majibu yenye kutosheleza.

(c) Watahiniwa wajengewe tabia ya kuthamini usomaji wa Qur'an na Hadithi za Mtume (s.a.w.) ili kuepuka kutoa tafsiri, mafunzo na maelezo ya Sura na Hadithi ambazo hazikidhi yale waliyoulizwa.

(d) Watahiniwa waelekezwe mbinu mbalimbali sahihi za uwasilishaji wa majibu katika mitihani. Ni muhimu sana wasisitizwe kusoma kwa makini na kuelewa kisha kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika mzizi wa swali.

Kiambatisho A

## MCHANGANUO WA MADA ZILIZOFANYIKA VIZURI NA HAFIFU CSEE 2015

**Karatasi ya Kwanza**

| Na. | Mada | Nambari ya swali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tarekh | 5 | 86.3 | Vizuri |
| 2 | Qur'an | 2 | 59.9 | Vizuri |
| 3 | Sunnah na Hadithi | 1 | 49.7 | Vizuri |
| 4 | Fiqh | 4 | 49.6 | Vizuri |
| 5 | Tawhiid | 3 | 44.3 | Wastani |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu** | | | **58.8** | |

**Karatasi ya Pili**

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Watahiniwa waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nambari ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1 | Fiqh | 7 | 71.3 | 54.6 | Vizuri |
| | | 8 | 55.4 | | |
| | | 9 | 37.2 | | |
| 2 | Tawhiid | 4 | 63.1 | 50.6 | Vizuri |
| | | 6 | 47.6 | | |
| | | 5 | 41.2 | | |
| 3 | Qur'an | 2 | 79.1 | 40.3 | Wastani |
| | | 3 | 36.5 | | |
| | | 1 | 5.4 | | |
| 4 | Tarekh | 10 | 28.8 | 23.9 | Hafifu |
| | | 11 | 20.4 | | |
| | | 12 | 20.4 | | |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu** | | | | **42.3** | |

Kiambatisho B

**UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALI MBALI**

**KARATASI YA KWANZA**

| **Na.** | Mada | 2014 | | | 2015 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Idadi ya maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi** | **Maoni** | **Idadi ya maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi** | **Maoni** |
| 1 | Sunnah na Hadithi | 1 | 70.4 | Vizuri | 1 | 49.7 | Vizuri |
| 2 | Fiqh | 1 | 71.1 | Vizuri | 1 | 49.6 | Vizuri |
| 3 | Qur'an | 1 | 53.7 | Vizuri | 1 | 59.9 | Vizuri |
| 4 | Tarekh | 1 | 46.7 | Wastani | 1 | 86.3 | Vizuri |
| 5 | Tawhiid | 1 | 9.4 | Hafifu | 1 | 44.3 | Wastani |

**KARATASI YA PILI**

| **Na** | Mada | 2014 | | | 2015 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Idadi ya maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi** | **Maoni** | **Idadi ya maswali** | **Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Alama 30 au Zaidi** | **Maoni** |
| 1 | Qur'an | 3 | 45.2 | Wastani | 3 | 40.3 | Wastani |
| 2 | Fiqh | 3 | 37.4 | Wastani | 3 | 54.6 | Vizuri |
| 3 | Tawhiid | 3 | 36.3 | Wastani | 3 | 50.6 | Vizuri |
| 4 | Tarekh | 3 | 15.8 | Hafifu | 3 | 23.9 | Hafifu |